JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA**

# Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya ya Mwaka 2023





**Mei, 2024**

# Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya ya Mwaka 2023

Imetayarishwa na
**Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya,**
**S.L.P** 80327, 8 Barabara ya Kivukoni,
11486 Dar es Salaam, **Barua pepe:** cg@dcea.go.tz
**Tovuti:** www.dcea.go.tz, **Instagram:** @dceatanzania
**Twitter :** @dceatanzania, **Facebook:** dceatz
**YouTube:** DCEATV, **Simu ya bure:** 119

**ISBN: 978 - 9912 - 9896 - 4 - 1**

**Imetayarishwa kwa mujibu wa Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Na. 5 ya mwaka 2015**

# YALIYOMO


**YALIYOMO ........................................................................................ iii**

**ORODHA YA MAJEDWALI ........................................................................ vii**

**ORODHA YA VIELELEZO .......................................................................viii**

**MAELEZO YA WAZIRI............................................................................. ix**

**DIBAJI ........................................................................................... xi**

**FAHARASA .......................................................................................xii**

**SURA YA KWANZA..............................................................................1**

**HALI YA DAWA ZA KULEVYA DUNIANI ...................................................1**

1.1 Utangulizi ........................................................................................1

1.2 Matumizi ya Dawa za Kulevya Duniani..................................................1

1.2.1 Bangi...............................................................................................2

1.2.1.1 Uhalalishaji wa Bangi na Athari zake.....................................................3

1.2.2 Dawa za Kulevya Jamii ya Afyuni ...........................................................4

1.2.3 Cocaine ..........................................................................................4

1.2.4 Dawa Tiba zenye Asili ya Kulevya..........................................................5

1.2.5 Dawa Mpya za Kulevya (New Psychoactive Substances - NPS)................5

1.2.6 Dawa za Kulevya Jamii ya Amphetamine (Amphetamine Type Stimulants-ATS) ...........................................................................5

1.2.7 Dawa za Kulevya na Jinsia.....................................................................7

1.2.8 Dawa za Kulevya na Maendeleo ya Teknolojia.........................................7

**SURA YA PILI....................................................................................9**

**MIKAKATI YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA NCHINI..................................................................9**

2.1 Utangulizi ....................................................................................9

2.2 Kudhibiti Upatikanaji wa Dawa za Kulevya (Supply Reduction)..............9

2.3 Kupunguza Uhitaji wa Dawa za Kulevya (Demand Reduction)................9

2.4 Kupunguza Madhara ya Matumizi ya Dawa za Kulevya (Harm Reduction) ....................................................................................10

2.5 Kuimarisha Ushirikiano wa Kitaifa, Kikanda na Kimataifa.....................10

**SURA YA TATU .................................................................................11**

**KUDHIBITI UPATIKANAJI WA DAWA ZA KULEVYA......................... 11**

3.1 Utangulizi.................................................................................... 11

3.2 Operesheni za Ukamataji wa Dawa za Kulevya......................................11

3.2.1 Bangi............................................................................................11

3.2.2 Mirungi .......................................................................................12

3.2.3 Heroin ........................................................................................14

3.2.4 Cocaine ......................................................................................14

3.2.5 Methamphetamine ......................................................................16

3.2.6 Ukamataji wa Vyakula vyenye Dawa za Kulevya...................................17

3.3 Watanzania waliokamatwa Nje ya Nchi ..........................................18

3.4 Udhibiti wa Kemikali Bashirifu na Dawa Tiba zenye Asili ya Kulevya ...18

3.4.1 Udhibiti wa Kemikali Bashirifu (Precursor Chemicals)...........................20

3.4.2 Ukaguzi wa Kemikali Bashirifu na Dawa Tiba zenye Asili ya Kulevya...20

3.4.3 Ufuatiliaji wa Matumizi na Uchepushwaji wa Dawa Tiba zenye Asili ya Kulevya.........................................................................................20

3.5 Mashauri ya Dawa za Kulevya ....................20
3.6 Uteketezaji wa Dawa za Kulevya ....................21
3.7 Maboresho ya Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya .22

**SURA YA NNE ....................23**

**KUPUNGUZA UHITAJI WA DAWA ZA KULEVYA (DEMAND REDUCTION) ....................23**

4.1 Utangulizi ....................23
4.2 Matumizi ya Dawa za Kulevya ....................23
4.3 Sababu zinazochangia Matumizi ya Dawa za Kulevya ....................23
4.4 Madhara ya Matumizi ya Dawa za Kulevya ....................26
4.4.1 Kiafya ....................26
4.4.2 Kijamii ....................26
4.4.3 Kiuchumi ....................27
4.4.4 Kisiasa na Kidiplomasia ....................27
4.4.5 Kimazingira ....................27
4.4.6 Unyanyapaa ....................28
4.5 Jitihada zilizofanyika katika Kupunguza Uhitaji wa Dawa za Kulevya....28

**SURA YA TANO ....................32**

**KUPUNGUZA MADHARA YANAYOSABABISHWA NA MATUMIZI YA DAWA ZA KULEVYA ....................32**

5.1 Utangulizi ....................32
5.2 Tiba ya Uraibu wa Dawa za Kulevya Katika Vitengo vya Afya ya Akili Nchini ....................32
5.3 Huduma ya Tiba Saidizi (MAT) kwa Waraibu wa Dawa za Kulevya .......37
5.4 Huduma za MAT Gerezani ....................37
5.5 Nyumba za Upataji Nafuu (Sober Houses) ....................37

5.6 Huduma za Kisaikolojia na Kijamii ........................................39
5.7 Asasi zilizowezeshwa na Mamlaka ........................................39
5.8 Faida ya Huduma za Upunguzaji Madhara kwa Waraibu ........................40

**SURA YA SITA ........................................................41**

**USHIRIKIANO WA KITAIFA, KIKANDA NA KIMATAIFA, KATIKA UDHIBITI WA DAWA ZA KULEVYA TANZANIA ........................................41**

6.1 Utangulizi ........................................................41
6.2 Ushirikiano wa Kitaifa ........................................................41
6.3 Ushirikiano wa Kikanda ........................................................43
6.4 Ushirikiano wa Kimataifa ........................................................43
6.5 Kazi nyingine zilizotekelezwa na Mamlaka ........................................43

**SURA YA SABA ........................................................46**

**CHANGAMOTO NA MIKAKATI YA BAADAYE ........................................46**

7.1 Utangulizi ........................................................46
7.2 Changamoto ........................................................46
7.3 Mikakati ya Baadaye ........................................................47

Kiambata Na. I ........................................................48
Kiambata Na. II ........................................................51

# ORODHA YA MAJEDWALI

**Jedwali Na 3.1:** Kiasi cha Bangi na Mirungi kilichokamatwa Nchini kati ya Mwaka 2014 hadi 2023 ......................................................... **12**

**Jedwali Na. 3.2:** Idadi ya Watuhumiwa wa Bangi na Mirungi waliokamatwa kati ya Mwaka 2014 hadi 2023......................................................... **13**

**Jedwali Na. 3.3:** Kiasi cha Heroin na Cocaine kilichokamatwa Nchini kati ya Mwaka 2014 hadi 2023 ......................................................... **14**

**Jedwali Na 3.4:** Idadi ya Watuhumiwa wa Heroin na Cocaine waliokamatwa Nchini kati ya Mwaka 2014 hadi 2023 ........................................ **15**

**Jedwali Na. 3.5:** Kiasi cha methamphetamine kilichokamatwa kati ya mwaka 2021 hadi 2023 ......................................................... **16**

**Jedwali namba 3.6:** Kiasi cha Kemikali Bashirifu zilizoiingizwa Nchini kuanzia mwaka 2017 hadi 2023......................................................... **18**

**Jedwali 3.7:** Kiasi cha Kemikali Bashirifu zilizozuiliwa kuingia Nchini Mwaka 2017 hadi 2023 ......................................................... **19**

**Jedwali Na.3.8.** Mwenendo wa Mashauri ya dawa za kulevya kwa Mwaka 2023.. **21**

**Jedwali Na. 3.9:** Takwimu za Uteketezaji wa Dawa za Kulevya kwa mwaka 2021 - 2023 ......................................................... **21**

**Jedwali Na. 5.1:** Idadi ya watu wenye Uraibu Waliopata Tiba kwenye Vitengo vya Afya ya Akili Nchini Mwaka 2023 ........................................ **33**

**Jedwali namba 5.2:** Idadi ya watu wenye uraibu waliosajiliwa katika vituo vya MAT nchini kuanzia Mwaka 2017 hadi 2023........................................ **35**

**Jedwali namba.5.3:** Vituo 16 vya MAT na idadi ya watu wenye uraibu waliosajiliwa kuanzia Mwaka 2017 hadi 2023........................................ **35**

**Jedwali Na. 5.4:** Asasi za kiraia zilizoibua watu wenye uraibu wa Dawa za Kulevya......................................................... **36**

**Jedwali na. 5.5:** Idadi ya watu wenye uraibu waliosajiliwa katika Nyumba za Upataji nafuu Mwaka 2019 -2023 Nchini ........................................ **38**

**Jedwali Na. 5.6:** Orodha ya Asasi za Kiraia zilizowezeshwa na Mamlaka mwaka 2023 ......................................................... **39**

# ORODHA YA VIELELEZO

**Kielelezo Na. 3.1:** Kiasi cha Bangi na Mirungi kilichokamatwa Nchini kati ya Mwaka 2014 hadi 2023 ....................................................................**12**

**Kielelezo namba 3.2:** Idadi ya Watuhumiwa wa Bangi na Mirungi waliokamatwa kati ya Mwaka 2014 hadi 2023 ......................................**13**

**Kielelezo Na.3.3:** Kiasi cha Heroin na Cocaine kilichokamatwa Nchini kati ya Mwaka 2014 hadi 2023 ....................................................................**15**

**Kielelezo Na 3.4:** Idadi ya Watuhumiwa wa Heroin na Cocaine waliokamatwa katika muongo mmoja wa Mwaka 2014 hadi 2024.................................**16**

**Kielelezo namba 3.6:** Kiasi cha Kemikali Bashirifu zilizoiingizwa Nchini kuanzia mwaka 2017 hadi 2023 ..................................................**18**

**Kielelezo namba 3.7:** Mwenendo wa Kiasi cha Kemikali Bashirifu zinazozuiliwa kuingizwa Nchini ..................................................**19**

**Kielelezo namba 5.1.:** Ramani ya Tanzania ikionesha Mikoa yenye Nyumba za Upataji Nafuu ....................................................................**30**

# MAELEZO YA WAZIRI

Serikali imeendelea kupambana na tatizo la uzalishaji, matumizi na biashara ya dawa za kulevya nchini. Mwaka 2023, umekuwa ni wa mafanikio makubwa katika historia ya mapambano dhidi ya dawa za kulevya kutokana na uwezeshaji uliofanywa na Serikali ya awamu ya sita chini Uongozi wa Jemedari wetu wa mapambano Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Jumla ya tani **1,965.34** za dawa za kulevya zilikamatwa kwa mwaka 2023 pekee ikiwa ni karibu mara saba zaidi ya kiasi kilichokamatwa tangu Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ianzishwe hapo mwaka 2017. Bangi iliendelea kukamatwa kwa wingi nchini ikiwa na tani **1,757.56** ikifuatiwa na mirungi tani **202.74,** heroin tani **1.31** na cocaine kilo **3.04**. Aidha, dawa za kulevya ambazo bado ni ngeni nchini ziliendelea kukamatwa, ikiwemo methamphetamine tani **2.41**, bangi kali maarufu kama '*skanka*' kilo **423.54** na paketi **17** za biskuti zilizochanganywa na bangi zenye uzito wa kilo **2.04**. Vile vile, Serikali imezuia uingizaji kinyume cha sheria wa tani **157.74** za kemikali bashirifu ambazo zingeweza kutumika kutengeneza dawa za kulevya.

Tiba ya uraibu wa dawa za kulevya imezidi kuimarika ambapo katika mwaka 2023 kulikuwa na jumla ya vituo **16** vya MAT vilivyohudumia watu **15,912,** nyumba za upataji nafuu maarufu kama sober house zilikuwa **56** zikihudumia watu **3,488**. Aidha, vitengo vya afya ya akili kwenye vituo vya huduma za afya viliwahudumia watu wenye uraibu wa dawa za kulevya wapatao **903,062.**

Elimu ili kuwakinga Watanzania wasijiingize kwenye matumizi na biashara ya dawa za kulevya iliendelea kutolewa kwa ushirikishwaji wa wadau. Mamlaka ilifanya makubaliano na TAKUKURU kutumia klabu ya kuzuia rushwa kupinga dawa za kulevya ili kukufikia taasisi za elimu ngazi ya wilaya. Aidha, Mamlaka imeendelea kushirikiana na asasi za kiraia katika kufikisha elimu kwa jamii ambapo

kwa mwaka 2023 asasi **63** zilitoa elimu kwa makundi mbalimbali ya kijamii.

Mamlaka ambayo ina miaka saba (7) tangu ianzishwe imefanikiwa kuongeza wigo wa udhibiti wa dawa za kulevya kwa kufungua ofisi kwenye kanda **tano** (5) zinazopatikana katika mikoa ya Arusha, Mbeya, Mtwara, Mwanza na Dodoma.

Mwisho, napenda kuwakumbusha kuwa vita dhidi ya dawa za kulevya inahitaji juhudi za pamoja. Kila mmoja atimize wajibu wake ikiwemo kutumia namba ya bure ya simu namba **119** kupata taarifa mbalimbali na kutoa taarifa ya wanaojihusisha na biashara ya dawa za kulevya.

**Mhe. Jenista J. Mhagama (Mb)**

***Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu)***

# DIBAJI

Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya huandaliwa kila mwaka kwa mujibu wa kifungu cha 60 cha Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Na. 5 ya mwaka 2015, kinachoielekeza Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kuandaa na kuwasilisha taarifa hiyo Bungeni. Lengo la taarifa hii ni kuwashirikikisha wananchi kufahamu hali halisi ya tatizo la dawa za kulevya na jitihada zilizofanywa na Serikali kudhibiti tatizo hilo.

Taarifa hii inabainisha hali ya tatizo la dawa za kulevya duniani, mikakati mikuu minne ya kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya nchini na utekelezaji wake. Mikakati hiyo ni kupunguza upatikanaji wa dawa za kulevya, kupunguza uhitaji wa dawa za kulevya, kupunguza madhara ya matumizi ya dawa za kulevya na kuimarisha ushirikiano wa kitaifa, kikanda na kimataifa katika udhibiti wa dawa za kulevya. Vile vile, taarifa hii imeainisha mafanikio, changamoto pamoja na kuorodhesha mapendekezo na mipango ya baadaye ya kukabiliana na tatizo la dawa za kulevya nchini.

Tatizo la dawa za kulevya ni mtambuka likihitaji ushirikishwaji wa wadau. Hivyo, taarifa hii inajumuisha shughuli mbalimbali zilizofanywa na wadau wa udhibiti wa dawa za kulevya wa ndani na nje ya nchi. Natoa shukrani zangu za dhati kwa wote walioshiriki kwa namna moja au nyingine ikiwemo waliowasilisha taarifa zao ambazo zimesaidia kufanikisha uandaaji wa taarifa hii.

**Aretas J. Lyimo**
***KAMISHNA JENERALI***
**MAMLAKA YA KUDHIBITI NA**
**KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA**

# FAHARASA

| | |
|---|---|
| **ATS** | Amphetamine Type Stimulants |
| **CDC** | U.S Centers for Disease Control and Prevention |
| **GF** | Global Fund |
| **HONLEA** | Heads of National Drug Law Enforcement Agencies |
| **IMTC** | Interministerial Technical Committee |
| **INCB** | International Narcotics Control Board |
| **MoU** | Memorandum of Understanding |
| **NPS** | New Psychoactive Substances |
| **TAA** | Tanzania Airports Authority |
| **TAKUKURU** | Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa |
| **TAMISEMI** | Tawala za mikoa na Serikali za Mitaa |
| **TANAPA** | Tanzania National Parks |
| **TCAA** | Tanzania Civil Aviation Authority |
| **THC** | Tetrahydrocannabinol |
| **TMDA** | Tanzania Medicines and Medical Devices Authority |
| **TRA** | Tanzania Revenue Authority |
| **UKIMWI** | Upungufu wa Kinga Mwilini |
| **UNODC** | United Nations Office on Drugs and Crime |
| **VVU** | Virusi vya UKIMWI |

# SURA YA KWANZA

# HALI YA DAWA ZA KULEVYA DUNIANI

## 1.1 Utangulizi

Sura hii imetumia dondoo za Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya Duniani ya mwaka 2023 ambayo imeelezea matumizi, biashara, uzalishaji na matibabu kwa waraibu. Aidha, sura hii inaonesha jinsi ukuaji wa sayansi na teknolojia ulivyoathiri matumizi, biashara, utoaji wa huduma kwa waraibu na udhibiti wa dawa za kulevya duniani.

## 1.2 Matumizi ya Dawa za Kulevya Duniani

Katika maeneo mengi duniani, kumekuwa na ongezeko kubwa la biashara na matumizi ya dawa za kulevya. Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya ya mwaka 2023 ilionesha kuwa mwaka 2021, takribani mtu mmoja kati ya kila 17 wenye umri kati ya miaka 15 hadi 64 ulimwenguni alitumia dawa za kulevya katika kipindi cha mwaka uliopita. Idadi iliyokadiriwa ya watumiaji wa dawa za kulevya kwa miaka kumi imeongezeka kutoka milioni 240 mwaka 2011 hadi milioni 296 mwaka 2021 ambalo ni ongezeko la asilimia 23.

Katika kipindi hicho, dawa za kulevya kama bangi, heroin, metamphetamine, cocaine pamoja na dawa tiba zenye asili ya kulevya zilitumika. Mwaka 2020, inakadiriwa kuwa watu milioni 36 walitumia dawa za kulevya jamii ya amphetamine (ATS), milioni 22 walitumia cocaine, na milioni 20 walitumia dawa aina ya “ecstasy”. Wanawake walitumia ATS zaidi na dawa tiba zenye asili ya kulevya wakati wanaume walitumia zaidi dawa jamii ya afyuni na cocaine.

Katika kipindi hicho, kulishuhudiwa ongezeko kubwa la uzalishaji, biashara na matumizi ya dawa mpya za kulevya (New Psychotropic Substances-NPS) kuwahi kutokea duniani. Matumizi ya dawa za kulevya yaliripotiwa kusababisha madhara ya kiafya kwa watumiaji na jamii, kama vile ongezeko la maambukizi ya virusi vya UKIMWI, magonjwa ya akili na homa ya ini. Hata hivyo, jitihada mbalimbali

zimeendelea kuchukuliwa ili kudhibiti uzalishaji, biashara, na matumizi ya dawa za kulevya, ikiwa ni pamoja na utoaji wa tiba kwa watu wenye uraibu wa dawa hizo.

### 1.2.1 Bangi

Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya Duniani ya mwaka 2023 ilionesha kuwa takribani watu milioni 219 walitumia bangi mwaka 2021, sawa na asilimia nne (4) ya idadi ya watu duniani. Idadi hiyo imeongezeka kwa asilimia 21 katika kipindi cha muongo mmoja uliopita. Hii inaonyesha kuwa matumizi ya bangi yanaendelea kuongezeka kwa kasi duniani kote. Matumizi ya bangi yameendelea kuwa ya juu zaidi Amerika Kaskazini, ambapo asilimia 17.4 ya watu wenye umri kati ya miaka 15 hadi 64 walitumia dawa hiyo mwaka 2021.

Barani Afrika taarifa ilionesha kuwa, Afrika Kaskazini ni kitovu cha biashara haramu ya bangi iliyosindikwa (cannabis resin) kuelekea Ulaya Magharibi. Matumizi ya bangi ni ya juu katika Afrika Magharibi na Kati na kufikia mwaka 2021, karibu asilimia 10 ya watu (milioni 30) waliripotiwa kutumia bangi katika kipindi cha mwaka 2020, hususan katika nchi ya Nigeria. Imeripotiwa kuwa Nchi nyingi barani Afrika zina uzalishaji wa bangi na kwamba imeendelea kuwa moja ya dawa inayosababisha athari kubwa miongoni mwa watu wanaopatiwa matibabu ya uraibu.

Katika mwaka 2021, asilimia 5.3 ya vijana wenye umri wa miaka 15 hadi 16 kote ulimwenguni (watu milioni 13.5) walitumia bangi. Hata hivyo, ripoti hiyo ilionesha kuwa athari za matumizi ya bangi kwa vijana ni kubwa zaidi kwa sababu ubongo wao bado unaendelea kukua, hivyo matumizi ya bangi yanaweza kuwa na athari kubwa na za muda mrefu, ikiwa ni pamoja na utegemezi unaotokea haraka zaidi kuliko kwa watu wazima. Aidha, taarifa hiyo hiyo ilibainisha ongezeko la kilimo cha bangi mwaka 2021, ingawa kukamatwa kwa bangi duniani kulionekana kupungua baada ya kufikia kiwango cha juu zaidi mwaka 2020. Zaidi ya hayo, mwaka 2021, asilimia 46 ya nchi zilionesha kuwa idadi kubwa ya magonjwa ya akili yalisababishwa na matumizi ya bangi. Hii inachangiwa na kuongezeka kwa uzalishaji na matumizi ya dawa hiyo, na asilimia 34 ya nchi zilionesha kuwa bangi ni dawa inayowasumbua zaidi, hasa kati ya wale wanaopata matibabu ya uraibu wa dawa za kulevya.

Mwaka 2011, ilithibitishwa kuwepo kwa aina mpya ya bangi ijulikanayo kama "creepy" ambayo ilitumika zaidi nchini Colombia. Aina hii mpya inasemekana kufanyiwa marekebisho ya kijenetiki na kuwa na kiwango kikubwa zaidi cha THC (tetrahydrocannabinol), hivyo kusababisha athari kubwa zaidi kwa watumiaji wa dawa hiyo. Taarifa hiyo inaonesha pia kwamba bangi hiyo mpya imeanza kuenea zaidi katika nchi za Amerika Kusini na inaweza kuenea hadi barani Afrika.

#### 1.2.1.1 Uhalalishaji wa Bangi na Athari zake

Baadhi ya nchi zimeendelea kuhalalisha kilimo cha bangi kwa matumizi ya kitabibu na yasiyo ya kitabibu. Hata hivyo, taarifa hiyo imetoa ufafanuzi kwamba hatua hii imekuwa na athari kubwa kwa watumiaji, usalama, ongezeko la uhalifu wa kimataifa unaovuka mipaka, na imepunguza juhudi za kimataifa za kupambana na matumizi haramu ya dawa hiyo. Kuna tofauti kubwa katika bidhaa za bangi, ambapo viwango vya kemikali inayosababisha uraibu, yaani THC, katika bidhaa kama vile biskuti na keki vimeongezeka hadi asilimia 60 kutoka kiwango cha asilimia tano (5).

Kwa mujibu wa taarifa kutoka Ofisi ya Umoja wa Mataifa inayoshughulikia Dawa za Kulevya na Uhalifu (UNODC), nchi zilizohalalisha matumizi ya bangi zimekuwa na ongezeko la idadi ya watu wenye matatizo ya akili na watu wanaojiua kutokana na matumizi ya bangi. Pia kuliijitokeza idadi kubwa ya watu waliohitaji matibabu hospitalini kutokana na matumizi ya dawa hiyo.

Barani Afrika, suala la matumizi ya bangi na dawa nyingine ya kulevya limekuwa likiongezeka kadri miaka inavyosonga mbele. Ingawa hakuna takwimu rasmi za kutosha zinazopatikana, kuna ishara za kuongezeka kwa matumizi ya bangi katika baadhi ya maeneo. Serikali nyingi barani Afrika zinaendelea kushughulikia tatizo hili kupitia mikakati ya kuzuia na kupambana na matumizi ya dawa za kulevya, pamoja na kutoa elimu kuhusu madhara yake kwa umma. Hata hivyo, kuna haja ya juhudi zaidi za kuelimisha na kuweka mikakati thabiti ya kudhibiti matumizi ya bangi na dawa nyingine za kulevya ili kulinda afya na ustawi wa jamii za kiafrika.

### 1.2.2 Dawa za Kulevya Jamii ya Afyuni

Taarifa ya Dawa za Kulevya Duniani ya mwaka 2023 ilionesha kuwa takribani watu milioni 60 walitumia dawa za kulevya jamii ya afyuni mwaka 2021, ikiwa ni asilimia 1.2 ya idadi ya watu duniani. Taarifa hiyo ilikadiria kwamba asilimia 31.5 ya watumiaji wa dawa za kulevya jamii ya afyuni walitumia heroin. Aidha, takribani asilimia 38 ya waraibu waliokuwa kwenye tiba, waliathiriwa zaidi na dawa za kulevya jamii ya afyuni. Hali hiyo ilisababisha theluthi mbili ya vifo vinavyosababishwa na kuzidisha kiasi cha matumizi ya dawa hizo (overdose). Katika nchi nyingi za Afrika, watumiaji wengi wa dawa za kulevya jamii ya afyuni hutumia zaidi heroin.

Afghanistan imeendelea kuwa mzalishaji mkubwa wa dawa jamii ya afyuni ikichangia kwa asilimia 80 ya dawa za jamii hiyo duniani katika mwaka 2022. Ingawa kumekuwa na ongezeko la uzalishaji wa mimea jamii ya afyuni katika nchi zalishaji kwa asilimia 26, kiwango cha uzalishaji duniani kimeonekana kushuka kutokana na kupungua kwa uzalishaji kwa asilimia 10 nchini Afghanistan kufuatia katazo la uzalishaji wa dawa hizo nchini humo. Hata hivyo, iliripotiwa kuwa njia ya Balkan ambayo huanzia nchini Afghanistan, Iran, Uturuki hadi nchi za Ulaya imeendelea kuwa njia kuu ya usafirishaji wa dawa za kulevya jamii ya afyuni. Aidha, ukamataji wa dawa zinazosafirishwa na watu binafsi ukiongezeka kwa mwaka 2022.

### 1.2.3 Cocaine

Kumekuwa na ongezeko la biashara na matumizi ya cocaine duniani na inahofiwa kusababisa ongezeko la masoko mapya ya dawa hii duniani. Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya Duniani ya mwaka 2023 ilionesha kuwa matumizi ya cocaine yaliongezeka kwa asilimia 0.5 mwaka 2022 ikilinganishwa na mwaka uliotangulia. Katika mwaka 2021, ilikadiriwa kwamba watu milioni 22 walitumia cocaine, sawa na asilimia 0.4 ya idadi ya watu duniani. Kiwango cha uzalishaji wa cocaine kilifikia rekodi ya juu zaidi mnamo mwaka 2021, kufikia takribani tani 2,304, ongezeko la tani 322 zaidi ya uzalishaji wa mwaka 2020 uliokuwa tani 1,982.

Taarifa hiyo ilionesha kuwa Amerika Kaskazini na Ulaya zimeendelea kuwa masoko makuu ya biashara ya cocaine. Aidha, biashara na usafirishaji wa cocaine kwa njia ya bahari uliendelea kushika kasi ambapo asilimia 90 ya kiasi cha cocaine kilichokamatwa kilikamatwa baharini. Vituo vya usambazaji na usafirishaji wa cocaine katika Pwani ya Magharibi vimeendelea kuongezeka, huku Afrika ikiwa kinara katika usambazaji wa dawa hizo kuelekea Mabara mengine. Hata hivyo ilionesha kuwa asilimia kubwa ya cocaine barani Afrika hukamatwa karibu na pwani. Maeneo yanayopatikana Afrika Magharibi hutumiwa kama eneo la kupitishia cocaine kutoka Amerika Kusini kuelekea Ulaya.

Hii inaonesha kuwa Soko la kimataifa la cocaine limepanuka zaidi, ikijumuisha nchi za Bara la Afrika, Amerika Kaskazini, Ulaya Magharibi na Asia, kutokana na ongezeko la uhitaji katika mabara hayo katika miongo miwili iliyopita. Matumizi ya cocaine yanaonekana kuongezeka kwa kasi barani Afrika, hususani Afrika Magharibi na Kusini, kama inavyodhihirishwa na idadi ya watu wanaopata matibabu ya dawa za kulevya.

### 1.2.4 Dawa Tiba zenye Asili ya Kulevya

Dawa tiba zenye asili ya kulevya ni dawa halali kwa ajili ya tiba ya maradhi mbalimbali hatahivyo, kutokana na asili yake ya kulevya, zikitumika bila kufuata ushauri wa daktari zinaweza kuleta uraibu kwa mtumiaji. Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya Duniani ya mwaka 2023 ilionesha kuwa zaidi ya tani 356 ya dawa tiba zenye asili ya kulevya zilizokusudiwa kutumika kinyume na taratibu zilikamatwa. Asilimia 47 ya watumiaji wa dawa tiba hizo zenye asili ya kulevya walikuwa ni wanawake.

Aidha, Ketamine ni dawa tiba yenye asili ya kulevya ambayo inaongoza kuchepushwa na kutumiwa kama dawa ya kulevya duniani, hususani katika nchi za Asia ya Mashariki na Kusini. Wachepushaji wamebadilisha muonekano wa dawa hizo ili kurahisisha usafirishaji wake. Pia, Ketamine imeongoza kwa kusababisha vifo na madhara mengi ya kiafya, duniani. Hadi sasa hakuna tiba maalumu kwaajili ya uraibu wa Ketamine.

Tramadol ni dawa tiba yenye asili ya kulevya ambayo matumizi yake yameongezeka kwa kasi katika miaka ya hivi karibuni, ikiikaribia morphine. Mwaka 2021, Bara

la Afrika lilikamata nusu ya Tramadol zilizokamatwa duniani. Aidha, dawa tiba aina ya Fentanyl imeongoza kwa kusababisha vifo kwenye nchi za Amerika ya Kaskazini ambapo kwa mwaka 2021, zaidi ya watu 90,000 walifariki kutokana na kuzidisha kiasi cha matumizi (*Overdose*).

### 1.2.5 Dawa Mpya za Kulevya (New Psychoactive Substances - NPS)

Dawa Mpya za Kulevya (NPS) ni dawa za kulevya ambazo zimetengenezwa kukwepa mkono wa sheria kwa kuiga kemikali zilizopo kwenye dawa za kulevya zinazodhibitiwa kimataifa kama vile bangi, heroin, mirungi na cocaine. Bangi na dawa tiba yenye asili ya kulevya aina ya ketamine zimeongoza kuigwa kemikali zake katika miaka ya hivi karibuni.

Taarifa hiyo ilionesha idadi ya dawa mpya zilizotambuliwa iliongezeka kutoka aina 555 mwaka 2020 hadi 618 mwaka 2021. Katika mwaka 2021 pekee, aina mpya za dawa za kulevya zipatazo 87 zilitambuliwa kwa mara ya kwanza. Hadi kufikia Disemba, 2022 dawa mpya za kulevya 1,184 zilitambuliwa duniani. Vilevile, jumla ya tani 19 za dawa mpya za kulevya zilikamatwa mwaka 2021, ambalo ni ongezeko la asilimia 40 kutoka mwaka 2020. Mara nyingi, NPS huuzwa kwenye mitandao ya siri (*Darkweb*), hivyo kurahisisha upatikanaji wake. Madhara ya dawa hizo ni makubwa na yamedhihirika zaidi katika nchi zilizoendelea.

### 1.2.6 Dawa za Kulevya Jamii ya Amphetamine (Amphetamine Type Stimulants-ATS)

Dawa zilizopo katika kundi hili ni pamoja na amphetamine, methamphetamine na ecstasy. Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya ya Dunia ya mwaka 2023 imeonesha ongezeko la matumizi ya dawa za kulevya za jamii hii duniani. Kwa mwaka 2021, watumiaji wa dawa za kulevya jamii ya ATS walikuwa milioni 36. Zaidi ya asilimia 45 ya watumiaji wa dawa hizo walikuwa ni wanawake.

Aidha, kumekuwepo na ongezeko la uzalishaji na usafirishaji wa dawa za kulevya aina ya methamphetamine nchini Afghanistan. Hii imekuja baada ya nchi hiyo kukataza uzalishaji wa mimea jamii ya afyuni. Watengenezaji wa methamphetamine pamoja na kutumia kemikali bashirifu aina ya Ephedrine na Pseudoephedrine wameanza kutumia pia kemikali bashirifu aina ya 1-phenly-2 propanone kuzalisha

dawa hiyo.

Pia, katika Taarifa hiyo imeonesha ukamataji wa zaidi ya tani 393 za methamphetamine, tani 114 za amphetamine na tani 10 za ecstasy. Nchi za Mashariki na Kusini mwa Asia pamoja na nchi za Amerika Kaskazini ziliongoza kwa ukamataji wa dawa ya kulevya aina ya methamphetamine. Kiasi kilichokamatwa katika nchi za Amerika ya Kaskazini ni sawa na asilimia 90 ya kiasi kilichokamatwa katika kipindi cha miaka mitano (5) kuanzia mwaka 2017 hadi 2021. Nchini Tanzania kwa miaka ya hivi karibuni, kumekuwa na ukamataji mkubwa wa dawa aina ya methamphetamine, hali inayotishia kuibuka kwa matumizi ya dawa hiyo hatari.

### 1.2.7 Dawa za Kulevya na Jinsia (matumizi ya dawa za kulevya na wanawake)

Tafiti zinaonesha kuwa, watumiaji wengi wa dawa za kulevya duniani ni wanaume. Katika kipindi cha miaka ya hivi karibuni kumekuwepo na ongezeko la wanawake walioingia kwenye matumizi ya dawa za kulevya. Wanawake wamekuwa wakitumia zaidi dawa tiba zenye asili ya kulevya (asilimia 47) zikifuatiwa na ATS (asilimia 45). Barani Afrika, matumizi ya dawa za kulevya yalitofautiana kati ya wanawake na wanaume, ambapo katika watumiaji bangi kulikuwa na wastani wa mwanamke mmoja kati ya wanaume tisa.

Wanawake wamekuwa wakiathirika zaidi na matumizi ya dawa za kulevya kutokana na maumbile yao ya kibaiolojia, tamaduni, jukumu la uzazi na athari za dawa kwa watoto ambao hawajazaliwa na wanaonyonyeshwa. Wanawake wenye uraibu wa dawa za kulevya ni tishio katika kuenea kwa VVU (mara 1.2 zaidi ukilinganisha na wanaume), magonjwa ya zinaa, kuongezeka kwa usafirishaji wa dawa za kulevya, ukahaba, kuharibika kwa mimba na watoto wachanga wenye matatizo ya akili. Hali hii hupelekea unyanyapaa na wanawake kutokudhuria tiba. Nusu ya watumiaji wa ATS walikuwa ni wanawake, lakini robo yao pekee walihudhuria huduma za matibabu.

### 1.2.8 Dawa za Kulevya na Maendeleo ya Teknolojia

Inakadiriwa kuwa watumiaji wa intaneti duniani ni asilimia 66 ya watu wote, na asilimia 59 kati yao hutumia mitandao ya kijamii. Miongoni mwa faida za teknolojia ni kurahisisha upatikanaji wa huduma za tiba ya uraibu kwa kutumia simu na

mawasiliano mengine ya kimtandao. Matumizi mabaya ya teknolojia huathiri faida za teknolojia na kurudisha nyuma maendeleo. Kwa mfano, Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya ya Dunia ya mwaka 2023 ilionesha ongezeko kubwa la uuzaji wa dawa za kulevya kwa njia ya mitandao ya siri (*Dark Web*) kwa kipindi cha miaka ya hivi karibuni. Zaidi ya robo tatu ya wanaume wanaotumia dawa za kulevya walinunua dawa hizo kupitia mitandao ya siri. Dawa mpya za kulevya (NPS) zinaongoza kuuzwa kwa njia hii.

Utafiti uliofanyika mwaka 2021 nchini Ireland ulionesha asilimia 64 ya mauzo ya dawa za kulevya yalifanyika kupitia mitandao ya kijamii (*social media*), asilimia 28 kupitia mitandao ya siri (*Dark Web*) na asilimia 8 kupitia maduka ya mitandaoni (*Online Shop*). Kwa mwaka 2022, asilimia 0.2 ya miamala iliyofanywa kwa njia ya fedha za kidijitali (*Crypocurrencies*) ilikuwa kwa ajili ya kuuza na kununua dawa za kulevya

# SURA YA PILI

# MIKAKATI YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA NCHINI

## 2.1 Utangulizi

Udhibiti na mapambano dhidi ya tatizo la dawa za kulevya nchini unatekelezwa kwa kuzingatia mikakati mikuu minne. Mikakati hiyo ni kudhibiti upatikanaji wa dawa za kulevya (supply reduction), kupunguza uhitaji wa dawa za kulevya (demand reduction), kupunguza madhara ya matumizi ya dawa za kulevya (harm reduction) na kuimarisha ushirikiano na wadau kitaifa, kikanda na kimataifa (national, regional and international cooperation). Mikakati hii imelenga kuwezesha utekelezaji wa Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya namba 5 ya mwaka 2015, pamoja na mikataba ya kimataifa ambayo Tanzania imeridhia.

## 2.2 Kudhibiti Upatikanaji wa Dawa za Kulevya (Supply Reduction)

Mkakati huu unalenga kudhibiti uingizaji, uzalishaji na usambazaji wa dawa za kulevya kwa kuzingatia masuala yafuatayo; Ukusanyaji na uchambuzi wa taarifa kuhusu biashara na matumizi ya dawa za kulevya; Ukamataji wa wafanyabiashara na dawa za kulevya; Udhibiti wa uzalishaji wa dawa za kulevya (Kilimo na Uzalishaji); usimamiaji wa Sheria ya dawa za kulevya nchini, Udhibiti wa uchepushwaji wa kemikali bashirifu na dawa tiba zenye asili ya kulevya pamoja na kuratibu uteketezaji wa dawa za kulevya.

## 2.3 Kupunguza Uhitaji wa Dawa za Kulevya (Demand Reduction)

Katika kutekeleza mkakati huu, elimu imetumika kama nyenzo muhimu ya kuijengea jamii uelewa wa tatizo la dawa za kulevya ili kuiepusha jamii hiyo isijiingize kwenye matumizi na biashara ya dawa hizo. Aidha, elimu imelenga kuihamasisha jamii kushiriki katika mapambano dhidi ya tatizo la dawa za kulevya. Kufanikisha utekelezaji wa mkakati huu Mamlaka inaratibu uelimishaji juu ya tatizo la dawa za kulevya katika jamii ikiwa ni pamoja na kuandaa Miongozo ya uelimishaji, kuwaandaa na kuwawezesha watoa elimu juu ya tatizo la dawa za kulevya, kuratibu

asasi zinazotoa elimu ya dawa za kulevya kwa umma, kuratibu uanzishwaji na uendeshaji wa klabu za kupinga dawa za kulevya na kuhuisha maudhui ya dawa za kulevya kwenye mitaala ya elimu.

## 2.4 Kupunguza Madhara ya Matumizi ya Dawa za Kulevya (Harm Reduction)

Matumizi ya dawa za kulevya husababisha madhara mbambali ikiwemo madhara ya kiafya kwa watumiaji na jamii kwa ujumla. Ili kupunguza madhara hayo Mkakati huu unalenga kutoa huduma za tiba, utengamao, ushauri na unasihi kwa waraibu wa dawa za kulevya. Maeneo ya msingi ya utekelezaji wa mkakati huo ni Kuratibu matibabu kwa waraibu wa dawa za kulevya; Kuandaa miongozo ya matibabu kwa waraibu wa dawa za kulevya; na Kufanya usimamizi shirikishi katika vituo vinavyotoa huduma za tiba, ushauri na unasihi kwa waraibu wa dawa za kulevya.

## 2.5 Kuimarisha Ushirikiano na Wadau Kitaifa, Kikanda na Kimataifa

Tatizo la dawa za kulevya ni suala mtambuka na ni uhalifu wa kupangwa unaovuka mipaka hivyo mapambano dhidi ya tatizo hili yanahitaji ushirikiano na nguvu za pamoja kuanzia ngazi ya kitaifa, kikanda na kimataifa. Katika kutekeleza mkakati yafuatayo yamezingatiwa; Kutekeleza mikataba na miongozo ya kitaifa, kikanda na kimataifa katika udhibiti wa dawa za kulevya; Kuhudhuria mikutano ya kisera na kisayansi kuhusu udhibiti wa dawa hizo; Kubadilishana taarifa na uzoefu baina ya mataifa mbalimbali kuhusu udhibiti wa dawa za kulevya pamoja na Kushirikisha wadau mbalimbali ndani na nje ya nchi katika mapambano hayo.

# SURA YA TATU

# KUDHIBITI UPATIKANAJI WA DAWA ZA KULEVYA

## 1.1 Utangulizi

Sura hii imeelezea mwenendo na jitihada zilizofanyika katika kudhibiti uzalishaji, uingizaji na usambazaji wa dawa za kulevya nchini hadi kufikia mwaka 2023. Katika kutekeleza mkakati huu Mamlaka kwa kushirikiana na vyombo vingine vya dola imefanikiwa kufanya operesheni mbalimbali za ukamataji, upelelezi, ufuatiliaji na uendeshaji wa mashauri ya dawa za kulevya, kutoa ushahidi mahakamani na kufanya uteketezaji wa dawa za kulevya. Aidha, imefanya ukaguzi katika maeneo mbalimbali ili kudhibiti uchepushaji wa kemikali bashirifu na dawa tiba zenye asili ya kulevya. Vile vile, Mamlaka ilifuatilia na kubaini mitandao ya kihalifu ya ndani na nje ya nchi inayojihusiha na biashara ya dawa za kulevya.

## 3.2 Operesheni na Ukamataji wa Dawa za Kulevya

Operesheni na ukamataji uliofanyika ulifanikiwa kukamata dawa za kulevya za mashambani aina ya bangi na mirungi pamoja na dawa za viwandani aina ya heroin, cocaine, methamphetamine na dawa tiba zenye asili ya kulevya kama ilivyoainishwa: -

### 3.2.1 Bangi


Katika mwaka 2023 kiasi cha tani **1,757.56** za dawa za kulevya aina ya bangi kilikamatwa kikihusisha watuhumiwa **8,803** kati yao wanaume **8,180** na wanawake **623.** ***(Rejea Jedwali Na. 3.1 na Kielelezo Na. 3.1).*** Aidha, katika kipindi hiki kumeibuka uingizaji na matumizi ya bangi mpya inayoitwa "skanka" ambayo inadhaniwa kuwa inazalishwa nchi za kusini mwa Afrika. Skanka ni mchanganyiko wa aina mbili za bangi, *Cannabis sativa* na *Cannabis indica*, ikiwa na kiasi kikubwa cha THC hivyo kuwa na athari kubwa zaidi kwa watumiaji.

### 3.2.2 Mirungi

Mirungi ni dawa ya kulevya ya mashambani ambayo pia imeendelea kuwa tatizo kwa mwaka 2023. Mwaka 2023, jumla ya tani **202.74** za dawa hii zilikamatwa zikihusisha watuhumiwa **1,179** kati yao wanaume **996** na wanawake **183. (*Rejea Jedwali Na. 3.1 na Kielelezo Na. 3.1.***

**Jedwali Na 3.1 Kiasi cha Bangi na Mirungi kilichokamatwa Nchini kati ya Mwaka 2014 hadi 2023**

| Mwaka | Bangi (Tani) | Mirungi (Tani) |
|---|---|---|
| 2014 | 81.30 | 15.74 |
| 2015 | 22.01 | 16.60 |
| 2016 | 68.23 | 21.64 |
| 2017 | 52.19 | 67.81 |
| 2018 | 24.30 | 8.96 |
| 2019 | 21.51 | 9.07 |
| 2020 | 13.23 | 11.80 |
| 2021 | 22.74 | 10.93 |
| 2022 | 20.58 | 15.23 |
| 2023 | 1,757.56 | 202.74 |





*Kielelezo Na. 3.1: Kiasi cha Bangi na Mirungi kilichokamatwa Nchini kati ya Mwaka 2014 hadi 2023*

Kiasi cha bangi tani 1,757.56 kilichokamatwa mwaka 2023 ni zaidi ya mara tano ya kiasi kilichokamatwa kwa miaka tisa iliyopita kuanzia mwaka 2014 hadi 2022 ambacho kilikuwa tani 326.09. Aidha, kiasi cha mirungi tani 202.74 kilichokamatwa kwa mwaka mmoja wa 2023, kinazidi kiasi cha mirungi kilichokamatwa kwa miaka tisa iliyopita (kuanzia mwaka 2014 hadi 2022) ambacho kilikuwa tani 177.78. Mafanikio haya yametokana na juhudi kubwa zinazofanywa na Serikali ikiwemo uwezeshaji, utashi wa kisiasa na ushiriki wa wananchi katika kutoa taarifa.

**Jedwali Na. 3.2: Idadi ya Watuhumiwa wa Bangi na Mirungi waliokamatwa kati ya Mwaka 2014 hadi 2023**

| Mwaka | Watuhumiwa - bangi | Watuhumiwa - mirungi |
|---|---|---|
| 2014 | 11,918 | 1,650 |
| 2015 | 13,275 | 1,780 |
| 2016 | 17,889 | 2,397 |
| 2017 | 11,528 | 1,797 |
| 2018 | 9,744 | 1,185 |
| 2019 | 8,865 | 1,170 |
| 2020 | 7,601 | 1,156 |
| 2021 | 9,484 | 1,395 |
| 2022 | 10,277 | 1,491 |
| 2023 | 8,803 | 1,179 |




*Kielelezo namba 3.2 Idadi ya Watuhumiwa wa Bangi na Mirungi waliokamatwa kati ya Mwaka 2014 hadi 2023*

### 3.2.3 Heroin


Mwaka 2023 jumla ya **tani 1.31** za dawa ya kulevya aina ya heroin ilikamatwa nchini ikihusisha watuhumiwa **196** kati ya hao wanaume **168** na wanawake **28.** Ukamataji wa kiasi hicho cha heroin ni mkubwa kuwahi kutokea katika historia ya mapambano dhidi ya dawa za kulevya nchini**.** (***Rejea Jedwali Na.3.3 na Kielelezo Na 3.3)***.

### 3.2.4 Cocaine

Katika mwaka 2023 operesheni zilizofanyika maeneo mbalimbali nchini zilifanikisha kukamatwa kwa kiasi cha kilo 3.04 za cocaine pamoja na watuhumiwa **32 (**wanaume **31** na mwanamke **mmoja**). Mwenendo wa ukamataji wa dawa hiyo unaashiria kuwa haipatikani kwa wingi hapa nchini. (***Rejea Jedwali Na.3.2 na Kielelezo Na 3.2***.

**Jedwali Na. 3.3: Kiasi cha Heroin na Cocaine kilichokamatwa Nchini kati kati ya Mwaka 2014 hadi 2023**

| Mwaka | Heroin (kg) | Cocaine (kg) |
|---|---|---|
| 2014 | 400 | 45 |
| 2015 | 64.75 | 17.79 |
| 2016 | 42.26 | 18.52 |
| 2017 | 185.56 | 4.14 |
| 2018 | 16.94 | 7.67 |
| 2019 | 55.35 | 10.34 |
| 2020 | 349.81 | 4.52 |
| 2021 | 1,124.52 | 0.811 |
| 2022 | 254.71 | 1.73 |
| 2023 | 1,314.28 | 3.04 |





***Kielelezo Na.3.3: Kiasi cha Heroin na Cocaine kilichokamatwa Nchini kati ya Mwaka 2014 hadi 2023***

Takwimu zinaonesha kuwa, mwaka 2023 kiasi cha heroin tani 1.31 ambacho ni sawa na kilogram 1,314.28 zilikamatwa. Ukamataji huu ni mkubwa kuwahi kutokea tangu nchi yetu ipate uhuru. Mafanikio haya yamechangiwa na juhudi kubwa zilizofanywa na vyombo vya ulinzi na usalama na ushiriki wa wananchi katika kutoa taarifa.

**Jedwali Na 3.4: Idadi ya Watuhumiwa wa Heroin na Cocaine waliokamatwa Nchini kati ya Mwaka 2014 hadi 2023**

| Mwaka | Watuhumiwa - Heroin | Watuhumiwa - Cocaine |
|---|---|---|
| 2014 | 584 | 351 |
| 2015 | 474 | 281 |
| 2016 | 716 | 263 |
| 2017 | 1,005 | 243 |
| 2018 | 463 | 148 |
| 2019 | 318 | 31 |
| 2020 | 428 | 80 |
| 2021 | 588 | 100 |
| 2022 | 409 | 122 |
| 2023 | 196 | 32 |




*Kielelezo Na 3.4: Idadi ya Watuhumiwa wa Heroin na Cocaine waliokamatwa kati ya Mwaka 2014 hadi 2024*

Kielelezo 3.4 kinaonesha mwaka 2023 idadi ya watuhumiwa waliokamatwa kwa kujihusisha na biashara ya heroin na cocaine ilipungua kutokana na ukamataji wa wafanyabiashara waliokutwa na kiasi kikubwa cha dawa hizo.

### 3.2.5 Methamphetamine

Mwaka 2023 jumla ya **tani 2.4** za dawa ya kulevya aina ya methamphetamine inayotengenezwa kwa kutumia kemikali bashirifu ilikamatwa nchini ikihusisha watuhumiwa tisa **(9),** kati yao wanaume watano **(5)** na wanawake wanne **(4).** Ukamataji wa kiasi hicho cha methamphetamine ni mkubwa kuwahi kutokea katika historia ya mapambano dhidi ya dawa za kulevya Nchini**.** (***Rejea Jedwali Na. 3.4 na Kielelezo Na. 3.4)***.

**Jedwali Na. 3.5: Kiasi cha methamphetamine kilichokamatwa mwaka 2021 - 2023**

| Na. | Mwaka | Methamphetamine (Kg) | Watuhumiwa |
|---|---|---|---|
| 1 | 2021 | 430.77 | 09 |
| 2 | 2022 | 0.97 | 02 |
| 3 | 2023 | 2,410.82 | 09 |

Takwimu zinaonesha kuwa dawa hii ilianza kukamatwa mwaka 2021 ambapo kiasi cha kilo **430.77**. Kiasi kilichokamatwa mwaka 2023 ni kilo **2,410.82** ambayo ni mara sita ya kiasi kilichokamtwa katika miaka miwili ya nyuma. Hii ni kutokana na juhudi kubwa za ukamataji wa biashara wa dawa hii zilizofanyika tangu kubainika hapa nchini.



***Dawa za kulevya aina ya heroin na methamphetamine zilizokamatwa mwaka 2023***

### 3.2.6 Ukamataji wa Vyakula vyenye Dawa za Kulevya

Matukio ya uwepo wa bidhaa za vyakula zinazotengenezwa kwa kutumia dawa za kulevya yameanza kushamiri hapa nchini. Kuanzia mwaka 2020 Mamlaka ilibaini na kukamata vyakula vilivyochanganywa na dawa za kulevya aina ya bangi katika matukio tofauti wakati wa utekelezaji wa operesheni zake. Vyakula vilivyobainika na kukamatwa ni pamoja na keki, biskuti, jamu na asali. Hali hii inaonesha kuwa tatizo hili linaendelea kuongezeka nchini na hasa ikizingatiwa wafanyabiashara hawa wenye nia ovu hutumia vyakula vinavyopendwa na watoto hivyo kuwaingiza kwenye matumizi ya dawa za kulevya bila kujua na hatimaye kuwa waraibu. Mwaka 2023, vyakula vyenye dawa za kulevya vilivyokamatwa ni **paketi 17** za biskuti zenye uzito wa kilogram 2.04 zikihusisha watuhumiwa wanne (04) wote wanaume.

## 3.3 Watanzania waliokamatwa Nje ya Nchi

Biashara ya dawa za kulevya ni miongoni mwa uhalifu wa kupangwa unaovuka mipaka. Wafanyabiashara wamekuwa wakitumia mbinu mbalimbali za usafirishaji wa dawa hizo kwenda nje ya nchi. Mwaka 2023, watanzania 26 walikamatwa nje ya nchi kwa tuhuma za kujihusisha na usafirishaji wa dawa za kulevya. Kwa mwaka 2022 Watanzania waliokamatwa nje ya nchi kwa kujihusisha na dawa za kulevya walikuwa 147, wanaume 136 na wanawake 11.

## 3.4 Udhibiti wa Kemikali Bashirifu na Dawa Tiba Zenye Asili ya Kulevya

### 3.4.1 Udhibiti wa Kemikali Bashirifu (Precursor Chemicals)

Kemikali bashirifu huingia nchini kwa ajili ya shughuli za uzalishaji mali kwenye sekta mbalimbali kama vile bidhaa viwandani, uchenjuaji madini katika migodi, kilimo, ujenzi, maji na katika kuboresha afya ya binadamu na mazingira. Kemikali hizi zisipodhibitiwa zinaweza kuchepushwa na kutumika kutengeneza dawa za kulevya. Kwa mujibu wa taarifa za Msajili wa Kemikali Nchini kiasi cha tani 28,780.8 na lita za ujazo 5,432,147.35 za kemikali bashirifu ziliingizwa nchini kwa kipindi cha mwaka 2023 kama inavyooneshwa kwenye jedwali.

**Jedwali namba 3.6: Kiasi cha Kemikali Bashirifu zilizoiingizwa Nchini kuanzia mwaka 2017 hadi 2023**


| Mwaka | Kiasi cha Kemikali | |
|---|---|---|
| | Tani | Lita |
| 2017 | 116,257.00 | 13,016,466.00 |
| 2018 | 1,534,064.00 | 11,247,555.00 |
| 2019 | 249,768.00 | 6,304,971.00 |
| 2020 | 96,062.44 | 4,256,161.00 |
| 2021 | 3,655.97 | 855,807.00 |
| 2022 | 11,389.00 | 5,711,266.00 |
| 2023 | 28,780.80 | 5,432,147.35 |

**Udhibiti wa Kemikali Bashirifu Kupitia Mifumo ya Kielektroniki ya Upashanaji Habari**

Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya hufuatilia taarifa mbalimbali za usafirishaji haramu wa kemikali bashirifu kupitia mifumo mbalimbali ya kitaifa na kimataifa. Katika kipindi cha mwaka 2023, kiasi cha **tani 159.3** na **lita 1,000** za kemikali bashirifu zilizuiliwa kuingia nchini kutokana na ukiukwaji wa taratibu. Kemikali hizo ni pamoja na Acetone, Toluene, Hydrochloric acid, Methylethylketone, Pseudoephedrine, Potassium Permanganate na Ethyl ether.

**Jedwali 3.7: Kiasi cha Kemikali Bashirifu zilizozuiliwa kuingia Nchini Mwaka 2017 hadi 2023**

| Mwaka | Kiasi (Tani) | Lita |
|---|---|---|
| 2017 | 250.1 | - |
| 2018 | 23.1 | - |
| 2019 | 43.6 | - |
| 2020 | 57.6 | - |
| 2021 | 120.3 | - |
| 2022 | 98.3 | 85 |
| 2023 | 159.3 | 1,000 |




*Kielelezo namba 3.7: Mwenendo wa Kiasi cha Kemikali Bashirifu zinazozuiliwa kuingizwa Nchini*

### 3.4.2 Ukaguzi wa Kemikali Bashirifu na Dawa Tiba zenye asili ya kulevya

Ukaguzi kwa ajili ya kufuatilia mwenendo wa biashara ya kemikali bashirifu na dawa tiba zenye asili ya kulevya ulifanyika katika maeneo 734 katika mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Mbeya, Mwanza, Songwe, Shinyanga, Dodoma na Kilimanjaro. Ukaguzi huo ulifanyika sambamba na operesheni maalumu ya kubaini na kuzuia uchepushwaji wa bidhaa hizo. Maeneo yaliyokaguliwa ni pamoja na kampuni zinazojihusisha na kemikali, maduka ya dawa tiba, maduka ya dawa za kilimo na mifugo, vituo vya afya, maghala ya kuhifadhi dawa tiba, kampuni za usafirishaji vifurushi, bandari kavu na vituo vya forodha vya mipaka ya Namanga, Tarakea na Holili, Horohoro, Kasumulu, Tunduma, Mutukula, Kabanga, Rusumo na Sirari.

Katika ukaguzi huo dawa tiba zenye asili ya kulevya aina ya Diazepam, Tramadol, Ketamine, Phenobarbitone, Zolpidem, Midazolam, Clonazepam, Alprazolam, Lorazepam, Pregabalin, Codeine na Methylphenidate zilikamatwa. Vile vile, Pethidine vidonge 143,345 sawa na kilogramu 1.96 na chupa ndogo 8,582 ambazo ni sawa na lita 61.67 zilikamatwa. Operesheni maalum ilifanikisha kukamatwa kwa watuhumiwa wanne (4) kwa kujihusisha na dawa hizo kinyume cha Sheria. Pia, ukaguzi ulibaini ukiukwaji wa taratibu za utunzaji wa kumbukumbu za matumizi ya kemikali bashirifu kwa baadhi ya kampuni za kemikali hali inayoweza kusababisha mianya ya uchepushwaji.

### 3.4.3 Ufuatiliaji wa Matumizi na Uchepushwaji wa Dawa Tiba zenye Asili ya Kulevya

Mamlaka kwa kushirikiana na TMDA, Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali na Baraza la Famasi ilifanya uchunguzi uliojumuisha famasi 130 na watu wenye uraibu 176 kutoka mikoa ya Arusha, Mbeya, Geita na Mwanza kwa lengo la kubaini endapo kuna uchepushwaji na matumizi holela ya dawa tiba zenye asili ya kulevya. Uchunguzi huo ulibainisha kuwepo kwa viashiria vya matumizi holela ya dawa tiba zenye asili ya kulevya hasa *Valium* na *Tramadol.*

## 3.5 Mashauri ya Dawa za Kulevya

Katika kipindi cha mwaka 2023 jumla ya mashauri **2,476** ya dawa za kulevya yalifunguliwa katika Mahakama mbalimbali nchini. Jumla ya mashauri yaliyotolewa maamuzi ni **1,005** kati ya mashauri hayo Jamhuri ilishinda mashauri **888** na kushindwa **117**. Mafanikio katika mashauri hayo yalitokana na kuimarika kwa mifumo ya upelelezi na uendeshaji mashtaka pamoja na ushirikiano miongoni mwa

wadau wa haki jinai. Aidha, mashauri 316 yaliondolewa Mahakamani kwa sababu mbalimbali. Mchanganuo wa mashauri ni kama inavyoonekana katika kielelezo Na 3.9

**Jedwali Na.3.8. Mwenendo wa Mashauri ya dawa za kulevya kwa Mwaka 2023**

| Dawa / Dawa Tiba | Mashauri yaliyoripotiwa | Mashauri yaliyofikishwa mahakamani | Mashauri yaliyoshinda | Mashauri yaliyoshindwa |
|---|---|---|---|---|
| Bangi | 1,059 | 1,059 | 447 | 79 |
| Mirungi | 1,179 | 1,179 | 406 | 36 |
| Heroin | 196 | 196 | 38 | 2 |
| Cocaine | 32 | 32 | 3 | - |
| Methamphetamine | 8 | 9 | - | - |
| Pethidine | 1 | 1 | - | - |
| Diazepam na Promethazine | 1 | 1 | - | - |
| **Jumla** | **2,476** | **2,476** | **888** | **117** |

## 3.6 Uteketezaji wa dawa za kulevya

Katika kipindi cha mwaka 2023 ulifanyika uteketezaji wa jumla ya ekari **2,389** za mashamba ya bangi katika mikoa ya Arusha, Morogoro na Mara. Jumla ya ekari **535** za mashamba ya mirungi katika Mkoa wa Kilimanjaro ziliharibiwa. Aidha, magunia **251** ya mbegu za bangi zilikamatwa na kuteketezwa katika Mikoa ya Arusha, Morogoro na Mara.

**Jedwali Na. 3.9 Takwimu za Uteketezaji wa Dawa za Kulevya kwa mwaka 2021 - 2023**

| Mwaka | Bangi | Mbegu za bangi | Mirungi | Mchanganyiko wa Bangi & mirungi | Heroin | Cocaine | Mchanganyiko wa Heroin & cocaine | Metha-mphetamine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2021 | Ekari 185 | - | Ekari 10.5 | - | - | - | - | Kilo 355 |
| 2022 | Ekari 179 | - | Tani 15.23 | Tani 2 | Kilo 621 | Kilo 15.3 | Kilo 199 | - |
| 2023 | Ekari- 2,389 na Tani 1.32 | Gunia 251 | Ekari - 535 | - | Kilo 25.4 | Kete 10 | - | - |



***Uteketezaji wa Dawa za kulevya aina ya Bangi, Heroin na Cocaine katika kiwanda cha Saruji cha Dangote.***

## 3.7 Maboresho ya Kanuni za Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya

Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Sura ya 95 na Kanuni zake zimekuwa zikifanyiwa maboresho kulingana na changamoto zinazojitokeza katika utekelezaji wake. Katika kipindi cha mwaka 2023, Kanuni za Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya za mwaka, 2016 zilifanyiwa maboresho kupitia Tangazo la Serikali **Na. 690** la tarehe **22 Septemba, 2023**. Maeneo yaliyofanyiwa maboresho ni pamoja na kuboresha taratibu za uchukuaji wa sampuli, kuongeza, kufuta baadhi ya tafsiri, kuongeza tafsiri za maneno, marekebisho ya jedwali la kwanza la Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Sura 95 kwa kuongeza idadi ya dawa tiba zenye udhibiti maalumu na maboresho ya fomu mbalimbali.

# SURA YA NNE

# KUPUNGUZA UHITAJI WA DAWA ZA KULEVYA (DEMAND REDUCTION)

## 4.1 Utangulizi

Kupunguza uhitaji wa dawa za kulevya ni mkakati wa pili kati ya mikakati mikuu minne ya udhibiti wa dawa za kulevya nchini. Mamlaka hutekeleza mkakati huu kwa kutoa elimu juu ya tatizo la dawa za kulevya kwa kushirikiana na wadau ili jamii isijihusishe katika matumizi ya dawa hizo. Elimu juu ya tatizo la dawa za kulevya hutolewa kwa jamii kwa njia mbalimbali ikiwemo semina, makongamano, vyombo vya habari, machapisho na maadhimisho ya kitaifa.

## 4.2 Matumizi ya Dawa za Kulevya

Dawa za kulevya ni kemikali ambazo zikitumika huathiri mfumo wa fahamu na kubadilisha fikra, hisia na tabia za mtumiaji. Bangi imeendelea kuwa ni dawa ya kulevya inayotumiwa na watu wengi nchini ikifuatiwa na heroin, mirungi na cocaine. Aidha, imebainika kuwepo kwa viashiria vya ongezeko la matumizi ya dawa tiba zenye asili ya kulevya kama Valium na Tramadol katika maeneo mbalimbali nchini. Vile vile, kumekuwepo na uingizwaji wa kiasi kikubwa cha dawa ya kulevya aina ya methamphetamine hali ambayo ni tishio kwa jamii kwani ina madhara makubwa na hayatibiki kirahisi.

## 4.3 Sababu zinazochangia Matumizi ya Dawa za Kulevya

Matumizi ya dawa za kulevya ni suala linaloisumbua jamii likisababishwa na sababu zifuatazo;

### a. Msukumo rika na kufuata mkumbo

Watumiaji wa dawa za kulevya huwa na ushawishi kwa marafiki, wenza au ndugu wasiotumia dawa hizo na kujikuta wakiwaingiza kwenye matumizi. Watu hao hufuata mkumbo ili kukubalika au kuwaridhisha watumiaji wa dawa za kulevya na kuthibitisha kuwa wako pamoja nao.

### b. Urahisi wa upatikanaji wa dawa za kulevya

Maeneo yaliyokithiri kwa kilimo na biashara ya dawa za kulevya kama vile bangi au mirungi huchochea jamii husika kujiingiza kwenye matumizi ya dawa hizo. Kupatikana kwa dawa za kulevya kiurahisi na kwa bei ndogo huifanya jamii kujihusisha na matumizi ya dawa hizo.

### c. Migogoro ya kifamilia

Kusambaratika kwa familia husababisha malezi duni hivyo kuzalisha watoto wenye tabia hatarishi ikiwemo matumizi ya dawa za kulevya kutokana na kukosa malezi bora. Watoto wanapokosa mwongozo na ufuatiliaji kutoka kwa wazazi au walezi wao hukosa mwelekeo wa maisha na huwa wepesi kujiingiza kwenye makundi hatarishi ikiwemo ya watumiaji wa dawa za kulevya.

### d. Ukuaji wa teknolojia

Biashara na matumizi ya dawa za kulevya vimekuwa vikifanyika na kutangazwa kwenye mitandao mbalimbali. Aidha, kuna matangazo ya biashara ya dawa za kulevya inayofanyika kwa mitandao ya wazi na kificho kwenye mitandao hiyo. Hali hiyo ikichangiwa na uhalalishaji wa matumizi ya dawa za kulevya hususani bangi huchochea matumizi ya dawa hizo bila kujali athari zake. Vilevile, ukuaji wa teknolojia umerahisisha ufichaji na usambazaji wa dawa hizo mfano uwepo wa bidhaa zenye bangi kama vile biskuti, kashata, shisha na keki.

### e. Kukosa stadi za maisha

Stadi za maisha ni maarifa yanayotarajiwa kumsaidia mtu kuishi vema kwa kujitambua uwezo na mapungufu yake na kuwa na malengo katika maisha. Maarifa hayo yakikosekana yanamfanya mtu kukosa uwezo wa kutambua na kutatua changamoto za maisha kwa usahihi. Hivyo, pale changamoto zinapojitokeza (mf. kupoteza ajira) hukimbilia kutumia vilevi mbalimbali kama suluhu ya changamoto zinazomkabili na kuishia kuwa mraibu wa dawa hizo.

### f. Imani potofu

Katika jamii kumekuwa na baadhi ya mila na desturi potofu ambazo huchochea matumizi ya dawa za kulevya. Kuamini kuwa ukitumia dawa za kulevya utaongeza ufanisi wakati wa kulima, kusoma, kuendesha gari, kuimba au kuongeza nguvu za

kiume ni imani potofu zisizo na tija zinazochangia watu kujihusisha au kuendelea kutumia dawa za kulevya. Pia, imani hizi zimeendelea kutumiwa na wauzaji wa dawa za kulevya kama njia ya kujipatia soko la dawa hizo pasipo kuwaeleza madhara yake. Hakuna tafiti za kisayansi zinazothibitisha ukweli wa imani hizo, hivyo kuishia kuwa ni imani potofu.

### g. Kukosa uelewa sahihi juu ya madhara ya dawa za kulevya

Kukosekana kwa uelewa sahihi juu ya madhara yatokanayo na matumizi ya dawa za kulevya husababisha jamii kujihusisha na matumizi ya dawa hizo kwa malengo mbalimbali ikiwemo kujifurahisha, kustarehe au kupunguza ukali wa maisha bila kufahamu madhara yanayotokana na matumizi ya dawa hizo.

### h. Matumizi ya dawa tiba zenye asili ya kulevya bila kufuata ushauri wa daktari

Dawa tiba zenye asili ya kulevya zinapotumiwa mara kwa mara na bila kufuata ushauri wa daktari husababisha uraibu. Watumiaji wa dawa tiba zenye asili ya kulevya kama vile Tramadol, Valium au Morphine wasipofuata maelekezo ya daktari huathirika na kupata madhara kama waraibu wa dawa nyingine za kulevya.

### i. Magonjwa ya afya ya akili

Magonjwa ya afya ya akili kama vile saikosisi (kuchanganyikiwa), msongo wa mawazo, sonona na kihoro husababisha mtu kujihusisha na dawa za kulevya kama njia ya kustahimili magonjwa hayo. Tafiti zinaonesha wagonjwa wa afya ya akili huambatana na matumizi ya dawa za kulevya hivyo kuongeza ukubwa wa tatizo la afya ya akili.

### j. Kurithi vinasaba vya uraibu

Kuwepo kwa vinasaba vya uraibu kwa wazazi huweza huchangia mtoto anayezaliwa kuwa na hali ya uraibu. Mara nyingi mtu anayerithi vinasaba vya uraibu akiishi kwenye mazingira yenye matumizi ya dawa hizo hupata uraibu.

## 4.4 Madhara ya Matumizi ya Dawa za Kulevya

Matumizi ya dawa za kulevya husababisha madhara mbalimbali; - kiafya, kijamii, kiuchumi, kimazingira na huchochea unyanyapaa. Madhara hayo yameainishwa kama ifuatavyo;

### 4.4.1 Kiafya

Matumizi ya dawa za kulevya huweza kusababisha magonjwa ya afya ya akili, moyo, ini, ngozi, figo, shinikizo la damu, kifua kikuu, kiharusi pamoja na uraibu unaosababisha kupata arosto kali. Mtumiaji anapotumia dawa za kulevya kwa njia ya kujidunga huwa katika hatari ya kupata na kueneza magonjwa ambukizi kama vile UKIMWI, virusi vya homa ya ini aina B na C. Aidha, matumizi ya dawa za kulevya hupunguza uwezo wa kufikiri, kutunza kumbukumbu na kufanya maamuzi sahihi. Pia, husababisha vifo vya ghafla hasa mtumiaji anapozidisha kiasi cha dawa za kulevya (overdose).

Watumiaji wa dawa za kulevya huwa katika hatari ya kupata saratani, madhara kwenye mfumo wa uzazi kama vile ugumba na utasa na upungufu wa nguvu za kiume. Kwa wanawake huvuruga mzunguko wa hedhi, huharibu mimba, husababisha kuzaliwa kwa watoto wenye uraibu wa dawa za kulevya, waliodumaa kimwili na kiakili, matatizo ya moyo, ulemavu wa viungo au kujifungua watoto njiti. Madhara mengine ya kiafya ni pamoja na kukosa usingizi, kukosa hamu ya kula, kuoza meno na upungufu wa kinga ya mwili dhidi ya maradhi. Kwa ujumla matumizi ya dawa hizi hupunguza umri wa kuishi wa mtumiaji kutokana na maradhi, uhalifu au kuzidisha kiasi cha dawa.

### 4.4.2 Kijamii

Kukithiri kwa vitendo vya kihalifu kama vile wizi, uporaji, ukahaba, utapeli, utekaji na mauaji kwa ajili ya kupata fedha za kununua dawa za kulevya au kwenye biashara ya dawa hizo haramu na kuathiri ustawi wa jamii husika. Matumizi ya dawa za kulevya huvuruga mahusiano katika familia na kusababisha kutengana kwa wazazi, kutelekeza familia hivyo watoto kukosa malezi bora na kukimbilia mitaani. Pia, matumizi ya dawa za kulevya kwa wanafunzi huathiri maendeleo ya

mwanafunzi shuleni na kusababisha utoro, utovu wa nidhamu na hata kuachishwa masomo.

Dawa za kulevya huchangia ongezeko la maradhi kwenye jamii isiyotumia dawa za kulevya kama vile maambukizi ya VVU, homa ya ini na kifua kikuu katika jamii kutoka kwa watumiaji ambao huwa na kiwango kikubwa cha maambukizi ya maradhi hayo. Pia, biashara ya dawa za kulevya huambata na biashara nyingine haramu kama vile silaha za magendo, biashara ya binadamu, kuweka watu rehani, uhalifu wa kimtandao, ujangili na madanguro. Iwapo mzazi atauawa au kufungwa kwa uhalifu wa kujihusisha na dawa za kulevya, familia yake hususani watoto watakosa matunzo ya mzazi husika. Aidha, matumizi ya dawa za kulevya husababisha ajali zinazoweza kuepukika ambazo husababisha ulemavu, vifo, uharibifu wa mali na miundombinu.

### 4.4.3 Kiuchumi

Uraibu wa dawa za kulevya hupunguza nguvu kazi ya taifa. Serikali huingia gharama zisizo za lazima kwa ajili ya ukamataji, tiba ya uraibu na utoaji elimu. Aidha, matumizi ya dawa za kulevya yanaambatana na uhalifu unaoweza kusababisha kufungwa gerezani hivyo, serikali kuingia gharama za uendeshaji wa kesi na kuwahudumia wafungwa hao badala ya kuelekeza rasilimali hizo kwenye shughuli za maendeleo. Vilevile, biashara ya dawa za kulevya husababisha mfumuko wa bei, kuongezeka kwa matabaka kati ya walionacho na wasionacho, umaskini, kukithiri kwa rushwa na utakatishaji wa fedha.

### 4.4.4 Kisiasa na Kidiplomasia

Kukithiri kwa biashara ya dawa za kulevya kunaweza kusababisha machafuko ya kisiasa, kuondoa tawala halali na kuweka tawala zinazotetea maslahi yao, kufadhili chaguzi ili kuwaweka viongozi wanaowataka wao, kuchafua taswira ya nchi na kufadhili magenge ya kihalifu.

### 4.4.5 Kimazingira

Matumizi ya dawa za kulevya kwa njia ya kujidunga husababisha uchafuzi wa mazingira pale vifaa vya kujidungia kama sindano ambazo huweza kuwa na vimelea vya maradhi zinapotupwa kwenye vichochoro, viwanja vya michezo, fukwe na

vituo vya daladala. Kilimo cha bangi huharibu mazingira kwa kusababisha ukataji miti kwenye misitu na kuharibu vyanzo vya maji. Wavutaji wa dawa za kulevya huchafua hewa kwa moshi unaotoka kwenye dawa hizo na kudhuru afya za watu walio karibu nao.

#### 4.4.6 Unyanyapaa

Waraibu wa dawa za kulevya wamekua wakinyanyapaliwa na hata kutengwa na familia zao pamoja na jamii kwa ujumla ambapo huitwa "mateja". Unyanyapaa huo huwafanya waraibu kutohudhuria kwenye vituo vya huduma za afya kupata matibabu, kukosa urithi na kusingiziwa makosa. Waraibu hushindwa kupata ajira hata pale wanapoacha matumizi ya dawa hizo. Unyanyapaa huo husababisha waraibu walioacha kutumia dawa za kulevya kurudi kwenye makundi ya wenzao kutafuta faraja, hivyo wanajikuta wanarejea katika matumizi ya dawa hizo (relapse).

### 4.5 Jitihada zilizofanyika katika kupunguza Uhitaji wa Dawa za Kulevya

Jamii iliendelea kuepushwa kujiingiza katika matumizi ya dawa za kulevya kwa kutoa elimu kwa kushirikiana na wadau kama ilivyoainishwa: -

#### i. Uzinduzi wa Mwongozo kwa ajili ya Klabu Shuleni na Vyuoni

Mamlaka kwa kushirikiana na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) iliandaa na kuzindua *Mwongozo wa Uelimishaji Kuhusu Rushwa na Dawa za Kulevya* utakaotumika kwenye klabu ya kupinga rushwa na dawa za kulevya Shuleni na Vyuoni. Pia, katika uzinduzi huo maafisa **58** wa TAKUKURU ngazi ya Mkoa na Maafisa wa Mamlaka Kutoka kanda walipata elimu ya namna ya kutumia mwongozo huo.

#### ii. Uelimishaji kwa Taasisi za Elimu

Mamlaka ilitoa elimu juu ya tatizo la dawa za kulevya kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari pamoja na wanavyuo kutoka katika vyuo vikuu na vya kati nchini. Takribani wanafunzi **100,000** walipata elimu hiyo katika shule na vyuo mbalimbali nchini

### iii. Maadhimisho ya Kitaifa

Siku ya Kupiga Vita Dawa za kulevya Duniani iliyoadhimishwa kitaifa jijini Arusha ambapo mgeni rasmi alikuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan. Maadhimisho mengine ya kitaifa yaliyotumika katika kutoa elimu ni pamoja na;- Maonesho ya 47 ya Biashara Kimataifa (Sabasaba) Mkoani Dar es salaam, Maadhimisho ya siku ya Kupinga Rushwa barani Afrika iliyofanyika Mkoani Arusha, Maonesho ya Siku ya Wakulima (Nanenane) Mkoani Mbeya, Uzinduzi wa Mbio za Mwenge uliofanyika Mkoani Mtwara, Maadhimisho ya Wiki ya Vijana yanayoambatana na Kilele cha Mbio za Mwenge wa Uhuru na Kumbukizi ya Kifo cha Mwalimu Nyerere mkoani Manyara, Maadhimisho ya Siku ya UKIMWI Duniani mkoani Morogoro na Maadhimisho ya Kitaifa ya Wiki ya Sheria jijini Dodoma.




***Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan akihutubia katika kilele cha Siku ya Kupiga Vita Dawa za Kulevya Duniani, jijini Arusha***



***Kamishna Jenerali akitoa Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya Nchini katika Maadhimisho ya Kitaifa ya Siku ya Kupinga Dawa za Kulevya Duniani***

### iv. Vyombo ya Habari

Katika kipindi cha kuanzia mwezi Januari hadi Disemba 2023, vipindi mbalimbali vya uelimishaji kuhusu tatizo la dawa za kulevya vilitolewa kupitia runinga, redio pamoja na uandishi wa Makala zinazotoa elimu kupitia magazeti, majarida, blogu na mitandao ya kijamii nchini. Aidha, wahariri **50** wa vyombo vya habari, waandishi wa habari **50** na waandishi **30** wa habari za kimtandao walijengewa uwezo katika kutoa taarifa zinazohusu udhibiti na mapambano dhidi ya dawa za kulevya.

### v. Taasisi za Serikali

Elimu juu ya tatizo la dawa za kulevya ilitolewa kwa Wakuu wa upelelezi wa mikoa wapatao **157**, watumishi **40** wa wilaya ya Shinyanga na Kahama, Timu ya Taifa ya wakimbiza Mwenge wa Uhuru **sita**, Watendaji wa Kata na Mitaa wa Ilemela Mwanza **168**, Maafisa michezo wilaya ya Kyela **20** na Wafanyakazi **100** wa Shirika la Ndege Tanzania.

### vi. Vyombo vya Ulinzi na Usalama

Mamlaka ilitoa elimu juu ya tatizo la dawa za kulevya kwa vyombo vya ulinzi na usalama ili kuongeza nguvu ya mapambano dhidi ya tatizo hilo. Takribani Maafisa uhamiaji wanafunzi **518** wa Chuo cha Raphael Kubaga, kilichopo Wilayani Mkinga, Mkoani Tanga, Maafisa wanafunzi **120** wa kikosi maalum cha magereza Ukonga mkoani Dar es salaam na Maafisa **20** wa TAKUKURU mkoa wa Arusha, walijengewa uwezo katika kukabiliana na dawa za kulevya kwenye majukumu yao ya kila siku. Vilevile, Mamlaka ilitoa mafunzo kwa waendesha mashtaka **178** kutoka mikoa ya Arusha (40), Kilimanjaro (38),Morogoro (35), Iringa (30) na Mara (35).

### vii. Majukwaa ya Kitaaluma

Mamlaka ilitoa elimu juu ya tatizo la dawa za kulevya katika mikutano ya kitaaluma ikiwemo Makatibu Mahsusi (TAPSEA) zaidi ya **5,000**, Wataalamu **610** wa Kada ya famasia na Wanahabari **130.**

### viii. Wadau wanaojihusisha na kemikali bashirifu na dawa tiba zenye asili ya kulevya

Katika kudhibiti uchepushaji wa kemikali bashirifu na dawa tiba zenye asili ya kulevya elimu ilitolewa kwa wadau **2,121** ambao wanajihusisha na kemikali bashirifu.

### ix. Uelimishaji uliofanywa na Asasi za Kiraia

Asasi za kiraia zimeendelea kushirikiana na Mamlaka katika kutoa elimu kwa makundi mbalimbali ya kijamii wakiwemo wanafunzi, wazazi, vijana walio nje ya mfumo rasmi wa elimu na watu wenye uraibu. Asasi hizi zimeweza kutoa elimu kwa jumla ya watu **2,838,630**. Jumla ya asasi **68** zilishirikiana na Mamlaka katika utoaji wa elimu katika mwaka 2023 (***Rejea kiambata namba I).***

# SURA YA TANO

# KUPUNGUZA MADHARA YANAYOSABABISHWA NA MATUMIZI YA DAWA ZA KULEVYA

## 5.1 Utangulizi

Matumizi ya dawa za kulevya yamekuwa ni moja ya tishio la afya ya jamii duniani. Upunguzaji wa madhara yanayosababishwa na matumizi ya dawa za kulevya ni moja ya mkakati muhimu katika kupambana na tatizo la dawa za kulevya nchini. Sura hii imeelezea utekelezaji wa mkakati wa tatu kati ya minne ya kudhibiti na kupambana na tatizo la dawa za kulevya kwa kipindi cha Mwaka 2023. Serikali hutoa huduma za upunguzaji wa madhara kwa watu wenye uraibu kupitia vituo vya tiba saidizi kwa kutumia dawa (Medically Assisted Therapy-MAT), vitengo vya afya ya akili vinavyopatikana kwenye baadhi ya vituo vya kutolea huduma za afya, nyumba za upataji nafuu (Sober Houses), huduma za unasihi na udungaji salama inayohusisha ugawaji wa sindano kwa wajidunga.

## 5.2 Tiba ya Uraibu wa Dawa za Kulevya Katika Vitengo vya Afya ya Akili Nchini

Serikali imeendelea kuboresha huduma za tiba kwa watu wenye uraibu wa dawa za kulevya katika kupunguza madhara yanayotokana na matumizi ya dawa hizo kwa kutoa tiba kwenye vitengo vya afya ya akili vilivyopo katika hospitali za wilaya, mikoa na rufaa nchini. Kwa kipindi cha mwaka 2023, jumla ya waraibu **903,062**, wanaume wakiwa **470,324** na wanawake **432,738** walipatiwa huduma ya tiba ya uraibu wa dawa za kulevya kama vile bangi, mirungi, heroin, cocaine na vilevi aina ya pombe na sigara katika vitengo hivyo.

Baadhi ya watu wenye uraibu walibainika kutumia dawa za hospitali zenye asili ya kulevya kama vile Valium, Pethidine na Tramadol, hali iliyosababishwa na kukosekana na kupanda kwa bei ya dawa za kulevya mitaani.

**Jedwali Na. 5.1: Idadi ya watu wenye Uraibu Waliopata Tiba kwenye Vitengo vya Afya ya Akili Nchini Mwaka 2023**

| Na. | Mkoa | Wanaume | Wanawake | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Dar es Salaam | 112,504 | 121,813 | 234,317 |
| 2 | Tanga | 21,074 | 14,183 | 35,257 |
| 3 | Arusha | 18,643 | 10,644 | 29,287 |
| 4 | Morogoro | 17,929 | 14,031 | 31,960 |
| 5 | Kilimanjaro | 10,908 | 13,412 | 24,320 |
| 6 | Kigoma | 12,241 | 17,122 | 29,363 |
| 7 | Mara | 17,386 | 8,383 | 25,769 |
| 8 | Mwanza | 30,239 | 20,430 | 50,669 |
| 9 | Kagera | 27,498 | 15,282 | 42,780 |
| 10 | Shinyanga | 13,700 | 14,885 | 28,585 |
| 11 | Geita | 12,004 | 9,543 | 21,547 |
| 12 | Manyara | 9,239 | 11,087 | 20,326 |
| 13 | Pwani | 29,471 | 32,843 | 62,314 |
| 14 | Dodoma | 18,290 | 10,280 | 28,570 |
| 15 | Singida | 9,066 | 4,633 | 13,699 |
| 16 | Tabora | 7,992 | 6,133 | 14,125 |
| 17 | Katavi | 9,839 | 9,017 | 18,856 |
| 18 | Rukwa | 5,763 | 9,022 | 14,785 |
| 19 | Njombe | 8,223 | 8,223 | 16,446 |
| 20 | Iringa | 13,621 | 12,617 | 26,238 |
| 21 | Mbeya | 19,428 | 16,899 | 36,327 |
| 22 | Ruvuma | 9,291 | 9,269 | 18,560 |
| 23 | Simiyu | 9,996 | 11,451 | 21,447 |
| 24 | Mtwara | 10,215 | 13,153 | 23,368 |
| 25 | Lindi | 6,630 | 8,224 | 14,854 |
| 26 | Songwe | 9,134 | 10,159 | 19,293 |
|  | **Jumla** | **470,324** | **432,738** | **903,062** |

## 5.3 Huduma ya Tiba Saidizi (MAT) kwa Waraibu wa Dawa za Kulevya

Tiba saidizi kwa kutumia dawa (MAT) imekuwa ni moja ya huduma bora ya kupunguza madhara na kusaidia watu wenye uraibu wa dawa za kulevya zenye asili ya afyuni hasa heroin pamoja na dawa tiba zenye asili ya kulevya mfano wa Tramadol, Pethidine na nyinginezo.

Huduma ya tiba saidizi kwa kutumia dawa ya Methadone na Buprenophine hutolewa katika hospitali za serikali nchini bila malipo. Watu wenye uraibu hupatiwa dawa na kuinywa au kumeza katika vituo husika chini ya uangalizi ya watoa huduma. Hata hivyo baadhi ya watu wenye uraibu waliokidhi vigezo hupatiwa dawa hiyo na kuitumia nyumbani chini ya uangalizi wa ndugu. Lengo la huduma hiyo ni kupunguza mlundikano vituoni, kupunguza wingi wa kazi kwa watoa huduma na kutoa fursa kwa waraibu wenye matatizo ya kijamii na mahitaji muhimu kama vile wajawazito, watumishi, watu wenye ulemavu na wenye magonjwa ya kuambukiza. Huduma ya MAT imekuwa ikitolewa pamoja na vipimo, matibabu ya magonjwa yanayoambatana na matumizi ya dawa za kulevya ya kifua kikuu, homa ya ini, pamoja na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI.

Wakati Mamlaka inaanzishwa mwaka 2017 kulikuwa na vituo vinne vinavyotoa huduma za MAT katika Jiji la Dar es Salaam na Mbeya vikihudumia watu wenye uraibu **4,307**. Hadi kufikia mwezi Disemba 2023 viliongezeka na kufikia jumla ya vituo 16 (vinne kati ya hivyo ni vituo vidogo - *satellite clinics*) katika mikoa tisa. Vituo hivyo vinapatikana katika mikoa ya Dar es salaam, Mwanza, Dodoma, Mbeya, Tanga, Arusha, Pwani (Bagamoyo na Kibaha), Songwe na Morogoro. Serikali imeendelea kuongeza huduma za MAT kwa kuanza ujenzi wa vituo vingine katika maeneo ya Chalinze Mkoa wa Pwani na Muheza Mkoa wa Tanga.

Vituo hivyo vinahudumia watu wenye uraibu **15,915** waliosajiliwa, ambapo **15,255** ni wanaume na **660** wanawake. Idadi ya watu wenye uraibu wa dawa za kulevya waliohudumiwa na MAT iliongezeka kutoka watu 4,307 Mamlaka inaanza kazi hadi 15,915 mwezi Desemba 2023, sawa na ongezeko la watu 11,608 **(rejea jedwali 1ifuatalo**).

**Jedwali namba 5.2: Idadi ya watu wenye uraibu waliosajiliwa katika vituo vya MAT nchini kuanzia Mwaka 2017 hadi 2023**

| Mwaka | | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi** | Me | 1,068 | 5,798 | 7,167 | 8,680 | 11,088 | 13,089 | 15,255 |
| | Ke | 38 | 406 | 471 | 508 | 587 | 607 | 660 |
| **Jumla** | | **4,307** | **6,204** | **7,638** | **9,188** | **11,675** | **13,696** | **15,915** |

**Jedwali namba.5.3: Vituo 16 vya MAT na idadi ya watu wenye uraibu waliosajiliwa kuanzia Mwaka 2017 hadi 2023**

| S/Na | Jina la Kituo | Mkoa | Jumla | Wanaume | Wanawake |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | MAT Hospitali ya Taifa ya Muhimbili | Dar es salaam | 3,743 | 3,603 | 140 |
| 2. | MAT Hospitali ya Rufaa ya Mwananyamala | Dar es salaam | 3,805 | 3,554 | 251 |
| 3. | MAT Hospitali ya Rufaa ya Temeke | Dar es salaam | 3,281 | 3,176 | 105 |
| 4. | MAT Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya | Mbeya | 527 | 508 | 19 |
| 5. | MAT Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Sekou Toure | Mwanza | 752 | 715 | 37 |
| 6. | MAT Hospitali ya Rufaa ya Wilaya, Tumbi Kibaha | Pwani | 490 | 485 | 5 |
| 7. | MAT Hospitali ya Wilaya, Bagamoyo | Pwani | 729 | 721 | 8 |
| 8. | MAT Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Mount Meru | Arusha | 668 | 634 | 34 |
| 9. | MAT Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Bombo | Tanga | 1,032 | 1,005 | 27 |
| 10. | MAT Hospitali ya Taifa ya Magonjwa ya Afya ya Akili, Itega | Dodoma | 598 | 576 | 22 |
| 11. | MAT Kituo cha Afya Tunduma | Songwe | 186 | 181 | 5 |
| 12. | MAT Gereza la Kihonda | Morogoro | 104 | 97 | 7 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 13. | MAT Gereza la Segerea | Dar es salaam | Usajili wa watu wenye uraibu katika vituo vidogo hivi hufanyika katika vituo mama vilivyopo katika mkoa wa Dar es salaam. | | |
| 14. | MAT Kituo cha Afya Round Table, Mbagala | Dar es salaam | | | |
| 15. | MAT Kituo cha Afya Tegeta | Dar es salaam | | | |
| 16. | MAT Hospitali ya Wilaya ya Vijibweni, Kigamboni | Dar es salaam | | | |
| | | | **15,915** | **15,255** | **660** |

Serikali imeendelea kuboresha huduma za tiba kwa watu wenye uraibu kwa kusimamia upatikanaji wa dawa ya methadone, buprenophine na vifaa tiba. Aidha, watoa huduma kwenye vituo vya MAT wamekuwa wakijengewa uwezo mara kwa mara ili kuongeza ufanisi. Huduma ya MAT imefanikiwa kutokana na ushirikiano na asasi za kiraia ambazo zimewezeshwa kuibua, kutoa rufaa na kupeleka waraibu katika vituo hivyo (**Rejea *Jedwali Na. 5.3*.**

**Jedwali Na. 5.4 Asasi za kiraia zilizoibua watu wenye uraibu wa Dawa za Kulevya**

| Na | Jina la Asasi | Na | Jina la Asasi |
|---|---|---|---|
| 1. | Life and Hope Rehabilitation Organization | 8. | Methadone Family Against Drug Abuse (MEFADA) |
| 2. | Organization of Youth Against Risk Behaviors (OYARB) | 9. | Kibao Salama Foundation |
| 3. | Gift of Hope Foundation | 10. | Integrated Rural Development Organization |
| 4. | Youth Volunteers Against Risk Behaviors (YOVARIBE) | 11. | Serve Tanzania (SETA) |
| 5. | Youth Community Rehabilitation (YCR) | 12. | Kimara Peer Educators |
| 6. | Peer to Peer Support Group | 13. | Foundation for Legal and Health Support |
| 7. | Mapambano ya Kifua Kikuu na UKIMWI Temeke (MUKIKUTE) | 14. | Steps Tanzania |

## 5.4 Huduma za MAT Gerezani

Serikali imechukua hatua ya uanzishaji huduma za tiba kwa watu wenye uraibu katika magereza ikiwa na lengo la kuwahudumia wafungwa, mahabusu pamoja na wananchi wanaozunguka maeneo ya gereza. Kituo cha MAT Gereza la Kihonda Mkoani Morogoro kilizinduliwa rasmi Novemba 2023 ikiwa ni kituo cha pili baada ya ufunguzi wa kituo cha MAT Segerea, Dar es Salaam Januari 2022.




*Kituo cha MAT Gereza la Kihonda, Morogoro*

## 5.5 Nyumba za Upataji Nafuu (Sober Houses)


Nyumba hizi zinamilikiwa na asasi za kiraia au watu binafsi kwa lengo la kutoa huduma za upataji nafuu kwa watu wenye uraibu wa dawa za kulevya. Mhusika hupatiwa huduma kwa kipindi cha miezi minne au zaidi. Afua zinazotolewa katika nyumba hizi ni tiba kwa kutumia hatua 12 za upataji nafuu, unasihi, msaada wa kisaikolojia na kijamii, tiba kwa njia ya mazoezi na kazi na matibabu ya kimwili na akili kwa kutumia wataalamu wa nje au ndani ya nyumba. Mamlaka huzisimamia na kuziratibu kwa kutumia *Mwongozo wa Uanzishaji na Uendeshaji wa Nyumba za Upataji Nafuu.*

Kuanzia mwaka 2019 hadi mwaka 2023 jumla ya watu **15,637** wenye uraibu walihudumiwa katika nyumba za upataji nafuu wanawake wakiwa asilimia **4.1** na wanaume asilimia **95.9**. Kwa mwaka 2023 jumla ya watu **3,488** wenye uraibu

walihudumiwa ambapo wanawake walikuwa 205 na wanaume **3,283. (rejea jedwali na. 5.4 na Kiambata II)**

**Jedwali na. 5.5 : Idadi ya watu wenye uraibu waliosajiliwa katika Nyumba za Upataji nafuu Mwaka 2019 - 2023 nchini.**

| Mwaka | | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi** | Me | 3,609 | 2,103 | 2,949 | 3,056 | 3,283 | **15,000** |
| | Ke | 74 | 74 | 160 | 124 | 205 | **637** |
| **Jumla** | | **3,683** | **2,177** | **3,109** | **3,180** | **3,488** | **15,637** |




*Kielelezo namba 5.1: Ramani ya Tanzania ikionesha Mikoa yenye Nyumba za Upataji Nafuu*

## 5.6 Huduma za Kisaikolojia na Kijamii

Kwa kuwa changamoto za kisaikolojia na kijamii zimechangia kuingiza watu kwenye uraibu wa dwa za kulevya, Taasisi za serikali, Asasi za kiraia na Mashirika ya kimataifa yamekuwa yakitoa huduma za msaada wa kisaikolojia na kijamii kwa watumiaji wa dawa za kulevya na jamii yake kama ndugu, jamaa na marafiki wa karibu. Katika huduma za msaada wa kisaikolojia na kijamii walengwa hupatiwa huduma za msaada wa kwanza wa kisaikolojia, unasihi, tiba za mabadiliko ya kitabia, tiba za familia, tathmini za afya ya akili na kuunganisha familia. Huduma hizi zimekuwa ni sehemu ya tiba ya uraibu wa dawa za kulevya kwa kuwa zinashughulikia kutibu kiini cha tatizo lililowaingiza kwenye uraibu.

## 5.7 Asasi zilizowezeshwa na Mamlaka

Mamlaka kupitia serikali na wadau mbalimbali imefanikiwa kuziwezesha asasi mbalimbali zinazofanya kazi ya utoaji elimu na upunguzaji madhara ya matumizi ya dawa za kulevya. Uwezeshaji uliofanywa na Mamlaka ni pamoja na fedha, mafunzo, miongozo na vifaa. Asasi zilizowezeshwa kifedha katika mwaka 2023 zimeainishwa kwenye jedwali lifuatalo; -

**Jedwali Na. 5.6. Orodha ya Asasi za Kiraia zilizowezeshwa na Mamlaka mwaka 2023**

| Na. | Jina la Asasi |
|---|---|
| 1 | Gift of Hope Foundation |
| 2 | Kibao Salama Foundation |
| 3 | Methadone Family Against Drug Abuse (MEFADA) |
| 4 | Mapambano ya Kifua Kikuu na UKIMWI Temeke (MUKIKUTE) |
| 5 | Organization of Youths Against Risk Behaviours (OYARB) |
| 6 | Peer to Peer Supporting Group |
| 7 | STEPS Tanzania |
| 8 | Tanzania Social Foundation for a Drug Free Generation (TSFDG) |
| 9 | Youth Community Rehabilitation (YCR) |
| 10 | Youth Volunteers Against Risk Behaviours (YOVARIBE) |
| 11 | Waungwana Group |
| 12 | Nazareth Kwaya |

## 5.8 Faida ya Huduma za Upunguzaji Madhara kwa Waraibu

Huduma za tiba na utengamao zina faida zifuatazo katika mapambano dhidi ya tatizo la dawa za kulevya:

i. Kupunguza matumizi na biashara ya dawa za kulevya na dawa tiba zenye asili ya kulevya;

ii. Kupunguza matendo ya uhalifu na uvunjaji wa amani;

iii. Kurejesha nguvukazi na kukuza uchumi kutokana na kuimarika afya na kutumia stadi za kazi zinazowapa fursa ya kujiajiri na kuajiriwa;

iv. Kupunguza maambukizi ya Virusi vya UKIMWI, Kifua kikuu na Homa ya Ini;

v. Kupunguza vifo kutokana na maradhi, uhalifu, kuzidisha kiasi cha matumizi ya dawa na magonjwa yasiyoambukiza.

vi. Kutoa fursa kwa watu wenye uraibu kupata tiba ya uraibu na magonjwa mengine ikiwemo magonjwa ya akili, msaada wa kisheria, rufaa mbalimbali, nk.

vii. Kuwarudisha watu wenye waraibu kwenye jamii zao na majukumu yao hivyo kuondoa unyanyapaa.

viii. Kupunguza mzunguko wa pesa chafu za wafanyabiashara wa dawa za kulevya.

# SURA YA SITA

# USHIRIKIANO WA KITAIFA, KIKANDA NA KIMATAIFA, KATIKA UDHIBITI WA DAWA ZA KULEVYA TANZANIA

## 6.1 Utangulizi

Tatizo la dawa za kulevya ni uhalifu wa kupangwa unaovuka mipaka ambao huendeshwa na mitandao ya kihalifu iliyopo maeneo mbalimbali duniani. Mkakati huu unaelezea jinsi serikali kupitia Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ilivyoshirikiana na wadau mbalimbali kitaifa, kikanda na kimataifa katika kukabiliana na tatizo hilo.

## 6.2 Ushirikiano wa Kitaifa

Mamlaka imekuwa ikishirikiana na Taasisi nyingine katika utekelezaji wa majukumu yake ambayo ni pamoja na utoaji elimu, utoaji wa huduma za tiba na utengamao kwa waraibu wa dawa za kulevya, kufanya operesheni na ukamataji, udhibiti wa uchepushwaji wa kemikali bashirifu na dawa tiba zenye asili ya kulevya, uendeshaji wa mashtaka na maboresho ya sheria.

Mamlaka ilishirikiana na wizara zenye dhamana ya Afya, Elimu, Mambo ya Ndani, Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, TAMISEMI, Sheria na Katiba, Fedha, Kilimo, Ujenzi, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Watu Wenye Mahitaji Maalum. Vilevile, ilishirikiana na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ya Zanzibar, Jeshi la polisi, Jeshi la Magereza, jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ), Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Idara ya Usalama wa Taifa, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Idara ya Uhamiaji, TANAPA, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Shirika la Posta Tanzania, Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA), Mamlaka ya Anga (TCAA), pamoja na Baraza la Famasi.

Mwaka 2023, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), ziliingia makubaliano (MoU) ya kushirikiana katika kuimarisha mapambano dhidi ya dawa za kulevya na rushwa nchini.




***Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na dawa za kulevya na Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa wakisaini Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano***

Aidha, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya imeingia Makubaliano ya Ushirikiano (MoU) na kampuni binafsi **109** zinazojihusisha na kemikali na dawa tiba kwa lengo la kudhibiti uchepushwaji wa kemikali bashirifu na dawa tiba zenye asili ya kulevya.

## 6.3 Ushirikiano wa Kikanda

Katika mwaka 2023, Tanzania imeendelea kupambana na tatizo la dawa za kulevya katika ngazi ya kanda ambapo imesaini Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano na Tume ya Kudhibiti Dawa za Kulevya Zambia (Drug Enforcement Commission – ZEC). Mamlaka ilishiriki Mkutano wa Tano wa Tume ya Ulinzi na Usalama inayojumuisha nchi yetu na Msumbiji, uliofanyika jijini Dar es Salaam.



***Sehemu ya washiriki wa Mkutano wa Tume ya Ulinzi na Usalama kati ya Tanzania na Msumbiji uliofanyika jijini Dar es salaam, tarehe 11 hadi 14 Septemba, 2023***

Vile vile, Mamlaka imewasilisha kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali rasimu ya hati ya makubaliano kati yake na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar (ZDCEA). Maeneo ya ushirikiano yaliyoainishwa ni pamoja na kubadilishana taarifa za kiintelijensia na uzoefu, kufanya operesheni za pamoja za udhibiti wa dawa za kulevya na kuwajengea uwezo watumishi.

## 6.4 Ushirikiano wa Kimataifa

Tanzania imeendelea kushiriki mikutano mbalimbali ya kimataifa kwa lengo la kubadilishana uzoefu, kushirikiana katika upatikanaji wa taarifa pamoja na kupanga mikakati ya pamoja katika udhibiti wa tatizo la dawa za kulevya barani Afrika na Duniani kwa ujumla. Tanzania ilishiriki mkutano wa Rota nchini Hispania ambao ulihusisha nchi wanachama wa Trilateral Planning Cell (TPC) na Jeshi la Maji la Umoja wa Ulaya (European Union Naval Force). Mkutano wa Wakuu wa Vyombo

vya Udhibiti wa Dawa za Kulevya Afrika (HONLEA) uliofanyika Abuja nchini Nigeria.

Vilevile, Mamlaka imeshiriki katika mikutano, semina na warsha mbalimbali zinazolenga kutekeleza mikakati ya udhibiti wa biashara ya dawa za kulevya nchi mbalimbali za Afrika ikiwemo Ivory Coast, Msumbiji, India, Singapore, Seychelles, Spain, Jamaica, Brazil na Marekani.

Pia, Mamlaka ilishiriki semina zilizoratibiwa na INCB kwa njia ya mtandao kuhusu; biashara ya dawa za kulevya na utakatishaji fedha; ufuatiliaji wa uteketelezaji wa mradi wa ushirikishwaji wa sekta binafsi katika kudhibiti uchepushwaji wa kemikali bashirifu; mashauriano ya pamoja kimataifa juu ya hatua za kuchukua katika kudhibiti ongezeko la kemikali zisizodhibitiwa ili zisitumike kwenye uzalishaji wa dawa za kulevya pamoja na jitihada za ushirikishwaji wa sekta ya viwanda katika kudhibiti kemikali bashirifu.

Aidha, Serikali imekuwa ikishirikiana na taasisi mbalimbali za kimataifa katika kupambana na kudhibiti tatizo la dawa za kulevya katika maeneo matatu ya kimkakati ya ukamataji, utoaji wa elimu na tiba ya uraibu wa dawa za kulevya. Baadhi ya wadau hao ni Drug Enforcement Adminstration (DEA) ya Marekani na National Crime Agency (NCA) ya Uingereza. Kutokana na ushirikano huo, Mamlaka ilifanikiwa kupata mafunzo na taarifa zilizofanikisha ukamataji mkubwa wa dawa za kulevya ambazo zilipitia baharini. Vilevile, taasisi za nje za CDC, Mfuko wa Dunia wa Kupambana na UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria (GF) zimeshirikiana na Serikali katika kupambana na tatizo la dawa za kulevya.

## 6.5 Kazi zingine zilizotekelezwa na Mamlaka

Pamoja na utekelezaji wa mikakati minne ya kupambana na dwa za kulevya ya elimu, tiba, ukamataji na ushirikiano na wadau, Mamlaka imetekeleza kazi zingine za kuimarisha mapambano dhidi ya dawa za kulevya kama ifuatavyo;-

i. Mamlaka kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) imeshawasilisha Waraka wa mapendekezo ya Sera ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya na kujadiliwa katika ngazi ya Makatibu Wakuu (IMTC).

ii. Ufunguzi wa Ofisi za Kanda na sasa kufikia tano nchini. Kanda hizo ni pamoja na Kanda ya Kati (Dodoma), Kanda ya Kaskazini (Arusha), Kanda ya Ziwa (Mwanza), Kanda ya Nyanda za Juu Kusini (Mbeya) na Kanda ya Pwani (Mtwara).

iii. Mamlaka imeanzisha Kituo cha Habari na Mawasiliano (*Information and Communication Center or Call Center*) kinachopatikana kupitia **Namba 119** kwa ajili ya kupata taarifa za biashara na matumizi ya dawa za kulevya pamoja na kutoa elimu kwa jamii kuhusu madhara ya biashara na matumizi ya dawa za kulevya ; na

iv. Mamlaka imeandaa Rasimu ya Mtaala wa Kufundishia Maafisa Wapya (*Training Curriculum for Basic Recruit Programme*) na Rasimu ya Kufundishia Maafisa waliopo Kazini (*Training Curriculum for Refresher Programme*).

v. Kuanza kwa ujenzi wa Jengo la Makao Makuu ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya katike eneo la Ndejengwa jijijni Dodoma.

vi. Uanzishwaji wa maabara ya uchunguzi wa sampuli za dawa za kulevya.

# SURA YA SABA

# CHANGAMOTO NA MIKAKATI YA BAADAYE

## 7.1 Utangulizi

Katika kipindi cha mwaka 2023 mafanikio makubwa yaliyopatikana yametokana na uwezeshaji mkubwa uliofanywa na Serikali pamoja na utashi wa kisiasa. Pamoja na mafanikio makubwa yaliyopatikana zipo changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa majukumu ya kupambana na dawa za kulevya nchini. Changamoto na mikakati imeainishwa kama ifuatavyo; -

## 7.2 Changamoto

Zifuatazo ni changamoto zinazokabili udhibiti na mapambano dhidi ya dawa za kulevya Nchini: -

i. Uelewa mdogo wa jamii juu ya tatizo la dawa za kulevya kama vile watoa huduma za afya, na viongozi ngazi za jamii.

ii. Mabadiliko ya teknolojia inayotumika katika biashara ya dawa za kulevya ikihusisha matumizi ya mitandao ya kijamii, vifaa vya kisasa kama ndege isiyokuwa na rubani, mitandao ya siri na fedha za kidijitali;

iii. Uhaba wa rasilimali watu na vitendea kazi vya kisasa katika kukabiliana na tatizo la dawa za kulevya Mfano Vifaa vya utambuzi wa wahalifu kama vile *scanner*, choo maalumu cha kutolea Dawa za Kulevya, Boti, 'Sniffer Dogs''pamoja na stoo za kutunzia vielelezo hasa vile vinavyopelekwa mahakamani;

iv. Jiografia ya nchi ikihusisha milima na maeneo zinapozalishwa dawa za kulevya yasiyofikika kirahisi, vipenyo vingi vya bahari na nchi kavu husababisha udhibiti wa dawa za kulevya kuwa mgumu;

v. Kuibuka kwa dawa mpya za kulevya (NPS) na kemikali bashirifu ambazo hazipo katika Sheria za Udhibiti wa Kitaifa na Kimataifa;

vi. Upungufu wa vituo vya kutolea huduma za tiba na utengamao kwa waraibu wa dawa za kulevya; na

vii. Kukosa ushirikiano kutoka kwa mashahidi huru;

## 7.3 Mikakati ya Baadaye

Mikakati ya kukabiliana na changamoto zilizoainishwa ni: -

i. Kuongeza wigo wa utoaji elimu kwa kushirikiana na wadau ili kuifikia jamii;

ii. Kuendelea kuwajengea uwezo wadau wanaoshiriki katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya ili kuongeza ufanisi katika udhibiti wa dawa hizo;

iii. Kuendelea kuboresha Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya;

iv. Kuendelea kujenga vituo vya huduma za tiba na utengamao katika maeneo yenye uhitaji;

v. Kuimarisha ushirikiano na mamlaka nyingine za udhibiti ndani na nje ya nchi pamoja na wadau wote kwa ujumla.

# Kiambata Na. I

**ORODHA YA ASASI ZILIZOFANYA KAZI YA UTOAJI ELIMU KWA MWAKA 2023**

| NA. | JINA LA ASASI |
|---|---|
| 1 | Action Plan Organization (APO) |
| 2 | Amani Sports Academy |
| 3 | Anti Alcoholism and Drug Addiction Organization (AADAO) |
| 4 | Bariadi Roots and Shoots Club |
| 5 | Bora Imani Children and Youth Foundation |
| 6 | Bright House of Change Organization |
| 7 | Care for All Organization |
| 8 | Chama cha wenye Ualbino |
| 9 | Changamoto ni Matumaini Foundation |
| 10 | Community on Mental Welbeing in Tz (COMWET) |
| 11 | Community Peers for Health & Environment Organisation (CPHEO) |
| 12 | Corner Stone Recovery Community |
| 13 | Drug Abuse Prevention Organization (DAPO) |
| 14 | Drug Abuse and Recovery Organisation (DARO) |
| 15 | De Porres Memorial Foundation |
| 16 | Foundation for Legal and Health Support (FLHS) |
| 17 | Foundation for Community Involvement (FCI) |
| 18 | Gift of Hope Foundation |
| 19 | Green Hope Organization |
| 20 | Health Aid and Care for the Future Foundation (HACFF) |
| 21 | International Organization of Good Templars (IOGT) |
| 22 | Tanzania Organization of Good Templars (T- OGT) |
| 23 | Juza Waste Pickers Initiative |

| NA. | JINA LA ASASI |
|---|---|
| 24 | Kibao Salama Foundation (KIBAFO) |
| 25 | Kibwena Community Development |
| 26 | Kimara Peer Educators and Health Promotors (Kimara Peers) |
| 27 | Kirumba Movement for Harm Reduction |
| 28 | Konga Halmashauri ya Tabora |
| 29 | Kurunzi ya Jamii |
| 30 | Life and Hope Rehabilitation Organization |
| 31 | Lindi Support Agency for Welfare (LISAWE) |
| 32 | Mapambano ya Kifua Kikuu na UKIMWI (MUKIKUTE) |
| 33 | Marafiki wa Walimu Geita |
| 34 | Matumaini Group |
| 35 | Methadone Family Against Drug Abuse (MEFADA) |
| 36 | Methadone Recovery Community Empowerment – (MRCE-TZ) |
| 37 | Mtwara Non-Governmental Organization Network (MTWANGONET) |
| 38 | Naweza Tena |
| 39 | Next Generation Keepers Tanzania (NGK Tz) |
| 40 | Ngao ya Jamii |
| 41 | NURGET Development in Tanzania (NDT) |
| 42 | Organization of Youth Against Risk Behaviours (OYARB) |
| 43 | Peer to Peer Support Group |
| 44 | Purple Heaven Foundation |
| 45 | Rukwa Association of NGOs (RANGO) |
| 46 | Recovery Brotherhood |
| 47 | Rondo Women Development Organization |
| 48 | Rukwa Association of Non-Government Organization (RANGO) |
| 49 | Soma kwa Furaha |
| 50 | Steps Tz |
| 51 | Tanga Recovery Community |

| NA. | JINA LA ASASI |
|---|---|
| 52 | Tanzania Community Empowerment Organization |
| 53 | Tanzania Social Foundation for a Drug Free |
| 54 | Tanzania Users and Survivors of Psychiatry Organization (TUSPO) |
| 55 | Tanzania Social Foundation for Drug Free Generation (TSFDG) |
| 56 | Tanzania Network of People who Use Drugs (TANPUD) |
| 57 | The Helpers Organization |
| 58 | Voice of Encouragement (VET) |
| 59 | Waungwana Family |
| 60 | Women and Child Vision (WOCHIVI) |
| 61 | Wounded Healers Organization |
| 62 | Youth Achievement Village in Tz (YAVT) |
| 63 | Youth Empowerment Society Tanzania (YES) |
| 64 | Youth Community Capacity Enhancement (YOCOCE) |
| 65 | Youth Community Rehabilitation |
| 66 | Youth Empowernment and Psychotherapy Aid Organization (YEPAO) |
| 67 | Youth Wings Organization |
| 68 | Youth Volunteers Against Risk Behaviours (YOVARIBE) |

## Kiambata Na. II

**ORODHA YA NYUMBA ZA UPATAJI NAFUU ZILIZOTOA HUDUMA KWA MWAKA 2023**

| Na. | Jina la Nyumba | Jinsia | Mkoa |
|---|---|---|---|
| 1 | Arusha Recovery Sober House | Me | Arusha |
| 2 | Arusha Women Recovery Sober House | Ke | |
| 3 | Olmotonyi Recovery House | Me | |
| 4 | Meru Recovery Sober House | Me | |
| 5 | Njiro Recovery Sober House | Me | |
| 6 | Njiro Women Recovery Sober House | Ke | |
| 7 | Usa River Recovery Sober House | Me | |
| 8 | Surrender for Freedom Treatment Centre | Me | |
| 9 | Mwangaza Sober House | Me | |
| 10 | Moshono Foundation Sober House | Me | |
| 11 | Northern Hill Sober House | Me | |
| 12 | New Life Sober House | Me | |
| 13 | Tasor Sober House | Me | |
| 14 | Zayn Hope House | Me | |
| 15 | Pillimissanah Sober House | Me | |
| 16 | Changamoto ni Matumaini | Me | Dar es Salaam |
| 17 | Drug Abuse Prevention Organization (DAPO) | Me | |
| 18 | Drug Abuse Prevention Organization (DAPO) | Ke | |
| 19 | Drug Free Tanzania – The Right Way Recovery House | Me | |
| 20 | Drug Free Tanzania – The Ties That Bind Us Recovery Center | Me | |
| 21 | Hope Again Rehabilitation and Wellness Foundation | Me | |
| 22 | MRC Tanzania Sober House – 1 | Me | |
| 23 | MRC Tanzania Sober House – 2 | Me | |
| 24 | MRC Tanzania Sober House – 3 | Me | |
| 25 | MRC Tanzania Sober House – 4 | Me | |
| 26 | MRC Tanzania Sober House – 5 | Me | |
| 27 | MRC Tanzania Women Sober House – 6 | Ke | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 28 | The Awaited Rehab Centre | Me | |
| 29 | Pillimissanah Sober House | Me | |
| 30 | Pillimissana Sober House (Women) | Ke | |
| 31 | Goodwill Sober House | Me | |
| 32 | Kilimanjaro Recovery Community Organization 1 | Me | Kilimanjaro |
| 33 | Kilimanjaro Recovery Community Organization 2 | Me | |
| 34 | Kilimanjaro New Vision and Sobriety 1 | Me | |
| 35 | Kilimanjaro New Vision and Sobriety 2 | Ke | |
| 36 | Mchaka Mchaka Recovery Center | Me | |
| 37 | Surrender For Freedom Treatment Centre | Me | |
| 38 | Serenity Gate Rehab (SGR) | Me | |
| 39 | Kilimanjaro Recovery Center- (Goodwill and Inspiration for Youth Vision Organization (GIYVO) | Me | |
| 40 | Courage On Recovery Foundation | Me | Tanga |
| 41 | Gift of Hope Foundation | Me | |
| 42 | Tanga Drug Free Organization | Me | |
| 43 | Ngao Recovery Center | Me | |
| 44 | Cornerstone Recovery Community | Me | Morogoro |
| 45 | Free at Last Sober House | Me | |
| 46 | New Vision Oof Life Society Sober House | Me | Pwani |
| 47 | Life and Hope Sober House | Me | |
| 48 | The Light of Miracle Organization - Women's Hope Rehabilitation ………. | Ke | |
| 49 | Mamaz and Papaz Sober House | Me | |
| 50 | Life and Hope Sober House | Me | Mbeya |
| 51 | MRC Mbeya Sober House – 8 | Me | |
| 52 | Pillimissanah Sober House | Me | Mwanza |
| 53 | Sobriety Forever Rehabilitation Centre | Me | Kagera |
| 54 | Still They Can Sober House | Me | Kigoma |
| 55 | Foundation for Alleviation of Drugs Addiction and Sufferings (FADAS) | Me | Iringa |
| 56 | MRC Tanzania Sober House – 7 | Me | Dodoma |

**Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya,**
**S.L.P 80327, 8 Barabara ya Kivukoni,**
**11486 Dar es Salaam Barua pepe: cg@dcea.go.tz**
**Tovuti: www.dcea.go.tz Instagram: @dceatanzania**
**Twitter: @dceatanzania Facebook: dceatz**
**YouTube: DCEATV Simu ya bure: 119**